TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA


**ELIMU MASAFA NA ANA KWA ANA**

# KISWAHILI

***TEWW $K_2$***

## MODULI YA KUMI NA MBILI

# Uchambuzi wa Mashairi



**Somo 12:1** Uhakiki wa Mashairi ya Cheke Cheka

**Somo 12:2** Uhakiki wa Mashairi ya Diwani ya Mloka

**Somo 12:3** Uhakiki wa Mashairi ya Malenga Wapya

# TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA
# ELIMU MASAFA NA ANA KWA ANA

## KISWAHILI

*TEWW $K_2$*

## MODULI YA KUMI NA MBILI
## Uchambuzi wa Mashairi

**Somo: 12:1 Uhakiki wa Mashairi ya Chekacheka**
**Somo: 12:2 Uhakiki wa Mashairi ya Diwani ya Mloka**
**Somo: 12.3 Uhakiki wa Mashairi ya Malenga Wapya**

# KISWAHILI
*TEWW $K_2$*

## MODULI YA KUMI NA MBILI
## Uchambuzi wa Mashairi

**Somo: 12:1 Uhakiki wa Mashairi ya Chekacheka**
**Somo: 12:2 Uhakiki wa Mashairi ya Diwani ya Mloka**
**Somo: 12:3 Uhakiki wa Mashairi ya Malenga Wapya**

Taasisi ya Elimu ya Watu Wazim Masomo ya Elimu Masafa na Ana kwa Ana

## YALIYOMO


| | | UKURASA |
|---|---|---|
| 12.0.1 | Utangulizi wa Moduli | |
| 12.0.2 | Malengo ya Moduli | |
| Somo 12.1 | Uhakiki wa Mashairi ya Chekacheka... ... ... | 1 |
| Somo 12.2 | Uhakiki wa Mashairi ya Diwani ya Mloka ... ... | 28 |
| Somo 12.3 | Uhakiki wa Mashairi ya Malenga Wapya ... ... | 58 |

## 12.0.1 UTANGULIZI WA MODULI

Ndugu mwanafunzi, katika somo lililopita umehitimisha mfululizo wa masomo ya uhakiki wa vitabu tele vya riwaya.

Unakaribishwa kuendelea na mchakato wa uhakiki katika utanzu wa ushairi. Kama zilivyokuwa moduli mbil zilizotangulia, moduli ya uhakiki wa vitabu teule vya ushairi umegawanyika katika masomo.Kila somo linabeba uchambuzi wa kitabu kimoja cha ushairi kifani na kimaudhui. Masomo hayo ni pamoja na: Uchambuzi wa Mshairi ya Chekacheka, Diwani ya Mloka na Malenga Wapya.

## 12.0.2 MALENGO YA MODULI

Baada ya kumaliza moduli hii utaweza:

- Kujibu maswali ya fasihi yatokanayo na vitabu teule;
- Kuhakiki vipengele vya fani na maudhui katika vtabu teule;
- Kutathmini kufanikiwa au kutokufanikiwa kwa waandishi wa vitabu teule; na
- Kuwa tayari kufanya mtihani wa mwisho wa (Kidato cha Nne) katika somo la Kiswahili.

**SOMO: 12.1**

# UHAKIKI WA MASHAIRI YA CHEKACHEKA

## YALIYOMO


| | | UKURASA |
|---|---|---|
| 12.1.3 | Utangulizi wa Kitabu ... ... ... ... ... ... | 3 |
| 12.1.4 | Sehemu ya Kwanza: Maudhui ... ... ... ... | 3 |
| 12.1.5 | Zoezi la Kwanza ... ... ... ... ... ... | 11 |
| 12.1.6 | Muhtasari wa Sehemu ya Kwanza ...... ... ... | 12 |
| 12.1.7 | Sehemu ya Pili: Fani ... ... ... ... ... ... | 13 |
| 12.1.8 | Zoezi la Pili ... ... ... ... ... ... ... | 21 |
| 12.1.9 | Muhtasari wa Sehemu ya Pili ... ... ... ... | 22 |
| 12.1.10 | Maswali ya Kutuma kwa Mkufunzi ... ... ... | 23 |
| 12.1.11 | Muhtasari wa Somo Lote ... ... ... ... ... | 24 |
| 12.1.12 | Majibu ya Mazoezi ... ... ... ... ... ... | 25 |
| 12.1.13 | Marejeo ... ... ... ... ... ... ... ... | 27 |

### 12.1.3 UTANGULIZI

Katika kitabu chake cha Mashairi ya Chekacheka mwandishi amejitahidi kuonyesha maisha halisi yaliyopo katika jamii zetu. Kama msanii mwingine yeyote, Theobald Mvungi ameandika kazi ambayo, kwa vyovyote vile, msomaji hubaini kuwa wanyonge wanaguswa sana na masahibu aliyoyaongelea na chanzo cha masahibu hayo. Aidha, mashairi yaliyo katika kitabu hiki yamejaa maadili kwa jamii.

### 12.1.4 SEHEMU YA KWANZA: MAUDHUI

Baada ya kupata utangulizi huo kuhusu kitabu cha *Mashairi ya Chekacheka*, sasa tuchambue maudhui yaliyomo. Kama kazi nyingine za fasihi mashairi nayo huhakikiwa kwa kuzingatia vipengele vyote vya maudhui. Katika maudhui tutaanza kuchambua dhamira, halafu ujumbe.

**Dhamira**

Mpendwa mwanafunzi, dhamira au mawazo yaliyomchochea mwandishi kuandika *Mashairi ya Chekacheka* ni mengi na yanafaa kujadiliwa kwa umakini sana. Hata hivyo, zipo dhamira anwai zilizojitokeza na tunazijadili katika kazi hii.

Miongoni mwa dhamira zilizojitokeza ni kusema ukweli, siasa, mapenzi, dini, uhusiano wa kimataifa, maisha na majonzi. Hapa tutaanza kuchambua dhamira moja moja kama inavyojitokeza katika kitabu hiki.

**Kusema Ukweli**

Mwandishi anajenga dhamira ya kusema ukweli bila woga. Hii inajidhihirisha katika shairi lake la "kazi yetu harakati" (Uk. 22), anapomsifia mwandishi Penina Mhando wa kitabu cha *Lina ubani*. Mwandishi anasema kuwa Mhando kasema ukweli kuhusiana na walaji majahili bila kuonyesha unafiki wowote. Hivi ndivyo inavyostahili kwa msanii anayeambatana na jamii yake. Mwandishi anasema:

*"Muhando kasema kweli, ile kweli ilo kali,*
*Ameweka dawa kali, kidonda kipate hali,*
*Kwa walaji majahili, dawa yao ni ukali,*
*Kwa kiziwi aelewe, ni vitendo umwonyeshe*

Ubeti huu unaonyesha wazi kuwa mwandishi anapenda na kuthamini ukweli na hii huenda ndiyo sababu kaamua kuzungumzia katika mashairi yake kwa mfano siasa bila woga wala kificho.

**Siasa**

Katika dhamira hii mwandish anazungumzia masuala yahusuyo siasa kwa jicho pevu. Chini ya mwavuli wa siasa mwandishi anayajadili masuala yafuatayo:-

**(i) Mfumo wa siasa wa Chama kimoja**

Mwandishi anajadili siasa ya mfumo wa chama kimoja. Kwa maoni yake mfumo huu uliwanyima watu uhuru wa kushiriki ipasavyo katika siasa ya nchi yao. Kwa mfano, katika shairi lake la "Taifa wamelizika" (Uk.2) katika ubeti wa saba (Uk.2 ub. wa 8) anasema:

*"Mezikwa demokrasia, chama kimoja ndo ngao,*
*Watu hawana nafasi, kutetea nchi yao,*
*Mawazo ya ukakasi, mawazo ya mtitio,*
*Wapenda jibu mkato, wale waoga wa hoja."*

Zaidi ya hayo, mwandishi anawaponda wale wote waliokuwa wanaogopa mfumo wa siasa wa vyama vingi. Anaona kwamba hao hawana lolote isipokuwa wanaogopa kuumbuliwa mara vyama vingine vitakapochukua madaraka. Anasema:

*"Waogopao vingi vyama, ni hofu ya kuumbuka,*
*maovu wanayafuma, kwa dharau na dhihaka,*
*Vyama vingi vingesema, na kutwaa madaraka,*
*Pasipo uhuru huo, utu uko mashakani, (Uk. 2, Ub. wa 8)*

Inaonekana dhahiri hili lilitungwa wakati Tanzania ilipokuwa chini ya mfumo wa chama kimoja cha siasa. Ndiyo maana mwandishi anaelezea kutoridhishwa kwake na hali iliyokuwepo nchini ambapo viongozi, na hata raia, walikuwa wanang'ang'ania mfumo wa chama kimoja, kwa visingizio kedekede. Lengo hasa la mfumo wa chama kimoja kama mwandishi anavyosema katika ubeti wa mwisho wa shairi hili, ni kuwafanya wananchi wawe wavivu kufikiri na hivyo kuwawezesha watawala kufanya mambo yao watakavyo huku wananchi wakibaki kupiga makofi tu.

Tangu mfumo wa vyama vingi vya siasa uanzishwe hapa nchini Tanzania, leo ni zaidi ya miaka kumi kuna mazuri na mabaya

tunayoyaona. Ukweli ni kwamba kila jambo zuri pia lina ubaya wake. Pamoja na migogoro michache ya kisiasa iliyojitokeza, bado mfumo wa vyama vingi vya siasa umeonyesha manufaa makubwa.

**(ii) Demokrasia**

Licha ya kujadili siasa ya mfumo wa chama kimoja, shairi la "Taifa wamelizika" (Uk.2) pia limejadili suala la demokrasia. Mwandishi anawaomba wabunge wa chama tawala (CCM) na wajumbe wa mikutano mbalimbali ya chama kutopiga blaablaa wawapo vikaoni. Hii ni kwa sababu demokrasia haina maana ya kuongea kwa nguvu na kwa kelele bila vitendo. Dhamira hii inakubaliana na hoja za watu mbalimbali ambao wamekuwa wakiwalalamikia wabunge kwa tabia yao ya kulalamika kidogo. Kusifu sana na kuunga mkono hoja zote ziletwazo bungeni kwani wao binafsi hawaoneshi kuyaangalia masuala yajadiliwayo kwa jicho pevu kabla ya kuchukua hatua ya kuyaunga mkono. Mwandishi anaona kwamba wabunge na wajumbe wa aina hii hawawakilishi raia waliowachagua bali huwakilisha nafsi zao. Wanachojali ni utukufu, furaha zao na siyo shida za raia wao.

**(iii) Suala la Kutetea Haki**

Mwandishi anamwomba Rais A.H. Mwinyi aliyekuwa madarakani wakati huo kuwa imara na kulinda moto aliouwasha ili usizimwe. Inaelekea moto anaouzungumzia mwandishi ni haki. Hivyo anaombwa awe mkali ili kuhakikisha kuwa haki inatendeka katika jamii. Katika shairi lake la "Mwinyi umewasha moto! Angalia usizimwe."(Uk.1) Mwandishi anasema:

> *"Tumaini la wanyonge, kuwa ipo Serikali,*
> *Ile nchi ya mazonge, ya wenye meno makali,*
> *Wanyang'anyao matonge, wanyonge hawana hali,*
> *Mwinyi ukiwa mkali, ndiyo raha ya raia."* *(Ub.1).*

Katika ubeti huu mshairi anamhimiza Rais kuwa mkali kwani nchi anayoiongoza inaonekana kuwa ni ya mazonge (matatizo).

Aidha, mwandishi anamshauri Rais ajihadhari na wale anaotarajia kuwanyang'anya madaraka kwani kitendo hicho si cha kuwafurahisha.

Mwisho, mwandishi anamkumbusha Rais kutazama nyuma alikotoka, aende mitaani azungumze na watu ili aweze kupata kero za watu na kuzishughulikia:

*"Mwinyi nenda mitaani, raia utawakuta,*
*Yao tia maanani, walaji wapigwe vita,*
*Tazama kila konani, kumbuka vita ni vita,*
*Jambo la mwisho adili, kweli ibaki ni kweli, (Ub.6)*

**(iv) Ufujaji wa mali ya umma**

Mwandishi anaonyesha kuwa fedha za Serikali au za mashirika ya serikali zinatumika isivyopaswa. Anaonyesha kuwa baadhi ya viongozi wanajikopesha na wengine wanajilipa mishahara na masurufu mazuri wanapokuwa kwenye shughuli za kiofisi wawapo nje ya vituo vyao vya kazi. Baadhi ya shughuli wanazojipangia nje ya vituo vya kazi siyo muhimu. Wanafanya hivyo ili tu wapate njia za kuzitafuna fedha za umma. Katika shairi lake la "Ni wapi Ushauri" (Uk.24) Mwandishi anasema:

*"Wanawe idadi sita, wakulima maarufu,*
*Pamba mahindi ufuta, tena wanawatiifu,*
*Fedha wanazitafuta, wanunue maradufu,*
*Mavuno yamo nyumbani, haya nayo mnunuzi."(Ub.3)*

**Ukasuku**

Katika shairi lake la "Tuambae Ukasuku (Uk. 3), mwandishi anatoa wito kuwa tusiwe kasuku. Kasuku huwa hana jipya bali kurudiarudia tu yale yaliyosemwa. Mwandishi anawashauri wasanii nao wasiwe kasuku, wawe na msimamo; wasiyumbishwe na hali zao za uchumi na kuandika yale yasiyoendana na hali halisi ya jamii zao. Hii ina maana kuwa mwandishi anawaasa wasisiishie kuwa vipaza sauti tu vya walio madarakani. Zaidi ya hayo, mshairi anawaonya wasanii wasilambishwe sukari wakasahau wajibu wao, wajibu wa kuielimisha na kuikosoa jamii:

*"Mshairi jihadhari, usishikwe kama fimbo,*
*Kwa kulambishwa sukari, ukaimba zao nyimbo,*
*Ukafikiri fahari, unakuwa chao chombo,*
*Kuwabeba huwa budi, na viatu utalamba." (Ub.6).*

**Ulanguzi**

Ulanguzi ni tatizo jingine lililoishughulisha akili na kalamu ya Theobald Mvungi. Analielezea kama tatizo lililoshamiri katika jamii zetu bila kuwepo viongozi wa kukemea. Anawauliza

viongozi wako wapi kutokana na kushamiri kwa tatizo hili huku wakitakiwa kuliona na kulitatua: "Mu wapi Nawauliza" (Uk.16).

*"Ulanguzi umeshona, suti umejivalia,*
*Na mkatazo hakuna, hapa kwetu Tanzania,*
*Kauli yenye hapana, ulanguzi kuzuia,*
*Imepotea kabisa, hairudi asilani."Ub.1).*

Anaendelea kusema:

*"Walanguzi wameshinda, mabao mbili kwa moja,*
*Wayala haya matunda, usingizi wa viroja,*
*Migongo imetupinda, wagongwaji kwa pamoja,*
*Walanguzi wanachama, ndio umoja ni nguvu." (Ub.3)*

Aidha, katika shairi hili mwandishi anawataka viongozi walio madarakani waamke na kukemea vitendo vya ulanguzi. Anasema.

*"Mlio madarakani, usingizi sasa basi,*
*Likizo hiyo acheni, ilivyo sasa ukwasi,*
*Hizo bei zuieni, bei ziwe za kiasi,*
*Msingoje vishindo, hizo njozi ziacheni." (Ub.5).*

Kwa upande mwingine, mwandishi ametuonyesha kuwa watu wenye dhamana serikalini na kwenye mashirika ya umma ndio vinara wa ulanguzi. Hutumia fedha waipatayo kununulia magari ya kifahari na kujenga majumba yenye thamani kubwa ikiwa ni pamoja na kuendesha maisha ya anasa. Mwandishi anashauri viongozi wa aina hii wachukuliwe hatua, anasema, katika shairi la "Mwinyi umewasha moto." (Uk.1)

*"......walaji hupendwa sana, na tuhuma zikizidi,*
*Amishiwa kwa jana, na akale kwa juhudi,*
*Walaji wanajuana, hawa dawa yao radi..." (Ub.5)*

**Mapenzi**

Dhamira hii imezungumziwa na mwandishi kupitia mashairi kadhaa. Katika shairi la "Njiwa kiumbe mtini" Uk.12), mwandishi anazungumzia dhamira ya mapenzi kwa kutumia lugha ya picha. Njiwa anafananishwa na mpenzi ambaye anaumiza moyo wa yule apendaye. Katika shairi hili mwandishi anaonyesha kuwa mapenzi ni kitu kinachohitaji mioyo miwili kuridhiana na kuwa pamoja. Anaonyesha malalamiko ya mmoja

wa wapenzi kuwa yule apendwaye (njiwa) hataki kuwa wazi. Kukubali au kukataa; mwandishi anasema:

*"Matawi nikiyakwea, njiwa hurukia kule,*
*Si kwamba anikimbia, ni mbinu zake teule,*
*Tabu kuniongezea, hata chakula nisile,*
*Njiwa kushuka hashuki, na mtini haondoki."* (Uk.2)

Aidha, mpenzi huyo anamtaka mwenzie abaini mateso ya usumbufu utokanao na mapenzi,

*"Unayofanya si kweli, njiwa acha tafrani,*
*Moyo waunyima hali, kwanini unauhini?*
*Rudi usiende mbali, moyo uwe afueni,*
*Njiwa hebu baini, moyo unavyoteseka."* (Ub. 4)

Shairi jingine linaloongelea masuala ya kimapenzi ni "Penzi lisilo heshima." (Uk.15) Katika shairi hili mwandishi anaonesha mapenzi yasiyo ya dhati (kweli). Mapenzi haya hujali fedha zaidi kuliko utu wa mtu. Mwandishi analalamika kuwa mapenzi ya fedha si yaheshima kwa kusema:

*"Karaha isio kima, na huu ndio usasa,*
*Moyo unanitetema, hali hiyo inatesa,*
*Penzi lisilo heshima, penzi ladai mapesa,*
*Dunia imegeuka, kichwa kiko miguuni."* (Ub.3).

Katika shairi hili mwandishi anaonyesha jinsi anavyokerwa na mtindo wa kugeuza mapenzi kuwa biashara, anaweka msisitizo katika ubeti wa tano mstari wa mwisho anaposema, "*mapenzi yasinadiwe kama mashati dukani.*"

Nalo shairi la "kimoyo" (Uk.12) linazungumzia jinsi mtu anavyoteseka au kuhangaika pale mpenzi wake anapougua, hasa kama hana fedha za matibabu. Mwandishi anasema tiba kwa mpenzi wake inahitaji fedha nyingi ambazo yeye hana uwezo wa kuzipata ingawa anampenda sana mpenzi wake. Anabainisha:

*"Tiba imekuwa tabu, kimoyo utaumia,*
*Tabibu amejaa gubu, fedha amezipania,*
*Kwa ufakiri natubu, chanzo tiba kukimbia,*
*Kimoyo u maradhini, na u kwangu fikrani." (Ub.3).*

**Dini**

Mwandishi wa *Mashairi ya Chekacheka* pia amegusia suala la dini na maadili yake katika jamii. Anaona kuwa dini ya kikristo imekumbwa na uozo wa kusisitiza fedha badala ya mafundisho mema ya kimaadili kama ilivyokuwa tangu enzi. Katika shairi la "Chanzo cha huo uozo" (Uk.25) Mwandishi anasema:

*"Nimeona upotofu, humu ukiristoni,*
*Upotofu wenye hofu, wahubiri mu kundini,*
*Mlei na Askofu, nyote mfanye makini,*
*Dini iwe maadili, msisitizo si fedha."*

Katika ubeti huu mwandishi anazungumzia suala la michango mingi kanisani. Ni kweli usiopingika kuwa hivi leo baadhi ya madhehebu ya kikristo pesa inawekwa mbele sana. Wakristo wanajikuta katika mazingira kama ya kulazimishwa kutoa badala ya kusisitiza suala la kuacha maovu (dhambi) na kumrudia Mungu, ambalo ndilo lengo kubwa la dini yoyote.

**Majonzi**

Mwandishi ametunga utenzi mmoja wenye kuwasilisha dhana hii ya majonzi na simanzi. Utenzi wa "Indira" (Uk. 18) unaelezea kifo cha aliyekuwa Waziri Mkuu wa India, Bibi Indira Gandhi. Katika utenzi huu mwandishi anaonyesha masikitiko yake kuhusu kifo cha kiongozi huyo Anaeleza wasifu wake kama mtetezi wa wanyonge na mwenye utu:

*"Ni vipi imetokea,*
*Umetengwa na dunia,*
*Mauti kukuchukua,......(Ub.2)*

*Twakuaga kwa lazima,*
*Kwetu ulikuwa mama,*
*Na sasa umetuhama,*
*Mtetezi wa wanyonge" (Ub.4)*

**Dhuluma**

Mwandishi anaonyesha kuwa katika harakati za maisha wapo watu wanaoishi kwa kuwatendea dhuluma wenzao. Anaonyesha kuwa katika jamiii zetu zilizojaa tabu bado wapo watu wenye tabia ya kuwakandamiza wenzao. Katika shairi "Utu umekuwa kima" (Uk.19) mwandishi anaonyesha kuwa kwa sasa utu umepotea.

*"Katika haya mazonge,*
*Yenye miba ya mkonge,*
*Kunyang'anyana matonge,*
*Mwenye nguvu ndiye mtu." (Ub.1)*

*"Dhuluma ndiyo hekima,*
*Utu umekuwa kima,*
*Hafai, huyo mnyama,*
*Jumlaye ni uhuru." (Ub.3)*

Mpendwa mwanafunzi, katika kitabu hiki dhamira nyingi zimejitokeza kupitia mashairi mbalimbali. Hizi zilizojadiliwa ni chache tu miongoni mwa zile zilizosadifiwa kitabuni. Unashauriwa kukisoma kitabu ili unufaike zaidi na kuyapata yale tusiyoyagusa. Aidha, shairi moja huweza kuwasilisha dhana zaidi ya moja (mawazo tofautitofauti) usifikiri kuwa umepotoka iwapo itatokea hivyo kwani fasihi hupata mwelekeo kulingana na jamii husika.

**Ujumbe**
Baada ya kuchambua baadhi dhamira zilizojitokeza katika *Mashairi ya Chekacheka,* sasa hebu tuangalie ni mafunzo gani tuyapatayo kutoka kitabu hiki. Kwanza, mwandishi anatufundisha kuwa daima tuwe jasiri katika kusema ukweli.

Pili, mwandishi anawataka viongozi wawajibike ili kuiondolea jamii adha zilizopo.

Tatu, tuepuke kuwa kasuku, kukariri na kuhubiri mambo ya majukwaani bila kupima uzito wa yasemwayo.

Nne, viongozi wa dini waepuke tamaa ya pesa badala ya kuhubiri neno la Mungu na maadili mengine.

Tano, tuepuke ubadhirifu wa mali ya umma, tusitumie nafasi tulizopewa kwa manufaa yetu binafsi.

Sita, mapenzi ya pesa ni hatari katika jamii, hivyo tuepuke kumpenda mtu kwa kwa kujali hali yake kiuchumi. Aidha katika suala la mapenzi tunapata ujumbe kuwa ni lazima iwepo ridhaa ya wenzi wote wawili.

Mwisho, ni vizuri kuwaenzi marehemu waliotutangulia kwa yale mema waliyoyafanya enzi za uhai wao.

## 12.1.5 ZOEZI LA KWANZA

*Jibu maswali yafuatayo kisha linganisha majibu yako na yale yaliyotolewa mwishoni mwa kijitabu hiki.*

1. Taja dhamira tano zipatikanazo katika kitabu cha *"Mashairi ya Chekacheka."*

   (i) ..................................................................................

   (ii) ..................................................................................

   (iii) ............................................... ........................

   (iv) ..................................................................................

   (v) ..................................................................................

2. Kwa kusoma *"Mashairi ya Chekacheka"* ni mafunzo gani tuyapatayo?

   (i) ..................................................................................

   (iii) ..................................................................................

   (iv) ..................................................................................

   (v) ..................................................................................

   (vi) ..................................................................................

### 12.1.6 MUHTASARI WA SEHEMU YA KWANZA

Ndugu mwanafunzi, katika sehemu hii ya kwanza tumechambua kipengele cha maudhui katika kitabu cha *Mashairi ya Chekacheka.*

Tumeona kuwa, ndani ya kipengele cha maudhui tunapata dhamira na ujumbe. Katika *"Mashairi ya Chekacheka"* twaweza kupata dhamira kadha wa kadha lakini hapa tumeziorodhesha baadhi tu.

Kusema ukweli, siasa ambamo tumeona kuna siasa ya vyama vingi, demokrasia, suala la kutetea haki na ufujaji wa mali ya umma, nyingine ni ukasuku, ulanguzi, mapenzi, dini, majonzi na dhuluma.

Aidha tumeangalia ujumbe unaojitokeza katika *Mashairi ya Chekacheka,* ambayo ni pamoja:- kututaka tuwe na ujasiri wa kusema ukweli, viongozi wawe mstari wa mbele katika kuyakabili matatizo yanayoisonga jamii, viongozi wawe wanapima uzito wa kauli zao majukwaani kabla ya kuzihubiri, viongozi wa dini wazingatie maadili ya kazi zao badala ya kuendekeza tamaa zao katika pesa, mwandishi anatoa ujumbe kuwa tuepuke ubadhilifu wa mali ya umma na kutotumia nafasi zetu katika kunufaisha nafsi zetu, tusitangulize pesa katika suala la mapenzi bali iwe ridhaa ya kila mmoja miongoni mwa wapenzi. Anahitimisha kwa kututaka tuwe na moyo wa kuthamini mchango wa marehemu waliotutangulia kwa kuyaenzi mema waliyoyafanya enzi za uhai wao.

## 12.1.7 SEHEMU YA PILI FANI

Mpendwa mwanafunzi, kazi yoyote ya fasihi huchambuliwa kwa kuzingatia vigezo vya fani na maudhui. Kama tujuavyo kwamba fani na maudhui ni pande mbili za sarafu moja, na ili kukamilisha kauli hiyo ni kwamba hakuna maudhui bila fani na hakuna fani bila maudhui. Hivyo basi, baada ya kuchambua maudhui ya kitabu, hatuna budi kuchambua kipengele cha fani.

Katika fani mwanafunzi ujiulize swali hili, je, mwandishi Theobald Mvungi ametumiaje vipengele vya fani katika kuisana kazi yake? Swali hili limelenga kujua muundo, mtindo, matumizi ya lugha, kama vilivyotumiwa na mwandishi. Tuanze kwa kuanglia kila kipengele.

**Muundo**

Kitabu cha *Mashairi ya Chekacheka* ni kitabu kidogo chenye mkusanyiko na mashairi na tenzi. Kitabu kina jumla ya mashairi ishirini na saba, na tenzi nne. Mwandishi hakuyapa namba mashairi yake na wala hakuyapanga katika makundi maalumu, bali ameyachanganya. Ni kazi ya msomaji au mchambuzi kuyapanga kadri atakavyoona inafaa. Mashairi haya yana muundo unaokubalika. Yamejengwa na beti zisizozidi kumi na zisizopungua mbili. Hivyo, yanasomeka na kueleweka kwa urahisi.

*Mashairi ya Chekacheka* ni ya muundo wa tarbia. Tarbia ni mashairi yanayojengwa kwa mishororo minne. Labda tujiulize, mchororo ni nini katika ushari? Mshororo huweza kugawanyika katika sehemu mbili au tatu au usigawanyike kabisa. Pale unapogawanyika, kila sehemu ya mshororo huitwa kipande. Ili kuweza kuelewa maana hiyo tuangalie mfano huu kutoka *Mashairi ya Chekacheka:* katika shairi la *"Moyo." (Uk.13).*

> *"Moyo nimekushauri, lakini umekaidi,*
> *Moyo kiburi hatari, mfanowe kama radi,*
> *Moyo umefumbata shari, unayakwepa marudi,*
> *Moyo ua mwilini mwangu, jirudi tuwe pamoja." (Ub.1)*

Shairi hili lina mishororo (mistari) minne. Mishororo yake imejengwa kwa vipande viwili. Kwa mfano, *Moyo nimekushauri* ni kipande kimoja, *lakini umekaidi* ni kipande cha pili.

Mfano wa mishororo inayojengwa na vipande vitatu ni shairi la *"Kimoyo"* ubeti wa 1 (Uk.12).

Pili, tatu na nne:

> *"Wewe kimoyo sikia, mbona unanipa taabu?*
> *Si mimi, wanionea, kwamba wewe yakusibu,*
> *Ni pole na kwambia, pole, sina matibabu,*
> *Kimoyo, sinilaumu, uwezo mekuwa haba."*

**Mtindo**

Mwandishi ametumia mtindo maalumu wa mashairi ya kimapokeo. Huu ni mtindo mkongwe wa uandishi wa mashairi unaotii kanuni za urari wa vina na mizani. Vina ni silabi za katikati na mwishoni zinazofanana katika kila mstari wa ubeti wa shairi. Vina katika mashairi ya kitabu cha *Mashairi ya Chekacheka* vinatofautiana toka ubeti hadi ubeti.

Kwa mfano, Shairi la "***Kweli uliojaa udi***"

> *"Moyoni nasikitika, kwa haya ninayoona,*
> *Kila jua likitoka, ya leo yazidi jana,*
> *Foleni kwenye maduka, ndio kazi ya maana,*
> *Akili yanichonota, kujilisha tumeshindwa."*
>
> *"Ni miaka ishirini, tangu aondoke bwana,*
> *Kwenda huko uvunguni, na asije hapa tena,*
> *Ila tulio nchini, ni lipi hasa la maana,*
> *Tuseme twafanikiwa, yaani tumefanyaje?"*

Vina katika ubeti wa kwanza ni "ka" na 'na' na katika ubeti wa pili ni 'ni' na 'na'. Hili linadhihirisha tofauti ya vina toka ubeti hadi ubeti.

Mizani ni dadi ya silabi katika kila mstari. Mfano, mizani katika mstari huu ni:

| | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mo | yo | ni | na | si | ki | ti | ka, | kwa | ha | ya | ni | na | yo | o | na |
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 |

Idadi ya mizani katika huu mshororo ni 16.

Mwandishi amedhihirisha umahiri wake wa umapokeo kwa kutumia mizani 16 kwa kila ubeti katika mashairi yote.

Kwa upande wa tenzi, mwandishi huyu ametunga tenzi zenye mizani nane nane kwa kila mstari. Zina urari wa vina vya mwisho, yaani ulinganifu wa silabi ya mwisho kwa kila mstari kama tunavyoona katika ubeti huu wa tenzi ya "Utu umekuwa kima." (Uk. 19).

| Ka | ti | ka | ha | ya | ma | to | nge, |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 |

| Ye | nye | mi | ba | ya | m | ko | nge, |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 |

| Ku | nya | ng'a | nya | na | ma | to | nge |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 |

| Mwe | nye | ngu | vu | ndi | ye | m | tu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 |

Hata hivyo tenzi za Mvungi hazina beti nyingi kama inavyostahili. Upungufu huu unakosesha sifa mojawapo ya tenzi katika tenzi zake.

Mwandishi ametumia mtindo tofauti katika shairi lake la "Mtoto asoriziki" (Uk.27) kwa kuweka alama ya mshangao kati ya ubeti wa kwanza na pili. Hata hivyo mtindo huu unaonekana katika shairi hili tu. Kwa mfano:

*Diwani nawatunuku, wazazi baba na mama,*
*Ndio raia wa huku, nchi iliorudi nyuma,*
*Raia wenye shauku, shauku ya kwenda hima,*
*Shauku mimba kamili, ya mtoto si riziki.*
*Wapi!*

*Robo karne imekwenda, shauku hutubani,*
*Watu wafunga mikanda, mema wakatumaini,*
*Wapi! Miaka ikenda, kumbe baadhi njamani,*
*Shauku wameiuza, tena kwa bei rahisi.*

Katika shairi hili neno *Wapi! Lipo katikati ya beti hizi mbili.*

Aidha katika mashairi ya kitabu hiki tunaona kituo au kibwagizo kinatofautiana kwa kila ubeti. Hakuna kibwagizo kinachorudiwa rudiwa kama tulivyozoea katika mashairi mengine.

**Matumizi ya Lugha**
Kama ilivyo sanaa ya mashairi, mwandishi huyu ametumia lugha ya kishairi inayojibainisha kwa matumizi ya lugha ya mkato, wakati mwingine kulazimika kudondosha baadhi ya herufi ili kupata idadi sawa ya mizani.

Kwa mfano, badala ya kusema:
"nimejaribu" (Uk.12) inakuwa "mejaribu", "usiniguse" (Uk.20) inakuwa "isiniguse", "utawapata" (Uk.10) inakuwa "tawapata."

Aidha, mwandishi amechanganya viungo vizuri vya lugha ili kuipa lugha yake mvuto na kuibua hisia nzito. Ametumia misamiati, misemo, tamathali za semi na hata, taswira.

**Msamiati**
Kaumu (Uk.17) = umati wa watu
Kuhodhi (Uk.17) = kumiliki
Tafrani (Uk.12) = vurugu, fujo
Barakala (Uk.2) = mtu anayejipendekeza pendekeza ili apate cheo au kitu
Kushahidi (Uk.15) = fanya kuwa imara au madhubuti
Rihi (Uk.4) = harufu nzuri ya chakula
Ufakiri (Uk.12) = umaskini kabisa (ufukara)

**Misemo**
1. Taifa wamelizika (Uk.2) = Taifa wamelihujumu
2. Msilambishwe viatu (Uk.2) = msiburuzwe ovyo
3. Kushika hatamu (Uk.17) = kushika madaraka

**Tamathali za semi**
Mvungi ametumia tamathali nyingi za semi zilizojibainisha waziwazi, ambazo ni:

**Tashbiha**
1. Watu sawa na kamasi (Uk.5)
2. Mlevi akakolea kama tumbaku ya tozo (Uk.2)
3. Mfanowe kama radi (Uk.13)
4. Hotuba zamiminika mfano wa maji bombani (Uk.2)
5. Tazama pale jikoni sawa kiwanda kidogo (Uk.16)
6. Utaliwa kama pumba (Uk.21)
7. Mila punje kama kuku (Uk.3)

**Sitiari**

(a) Nchi wamefanya kuwa kuti (Uk. 2)

(b) ......... Maisha ni safari (Uk. 13)

(c) .......... Sisi ni miamba gogo (Uk. 5)

**Tashhisi**

1. Moyo unasemekana kuwa na kiburi unashauri lakini unakaidi (Uk.13).
2. Moyo unaambiwa ujifunze busara ili uwe ndio taa yake (Uk.13).
3. Moyo anaaswa usiwe na jeuri (Uk.13)
4. Ulanguzi umeshona suti (Uk.16)
5. Njiwa akitabasamu (Uk.12)

**Tashititi**

Tamathali hii nayo imetumiwa na mwandishi katika *Mashairi ya Chekacheka*. Kwa mfano shairi la Mtoto a so riziki (Uk. 26) ni tashititi kwa wale walioko madarakani (Uk. 26).

**Takriri**

Katika ushairi takriri ni kujirudia kwa silabi, neno au mstari.

**Takriri vina**

Takriri vina inajidhihirisha wazi katika kitabu hiki kwa vile vina katika mashairi haya yana ulinganifu wa vina vya kati na vya mwisho kwa kila mstari kwa mfano Shairi la "Chai" (Uk.11).

*Chai imeninogea shairi naitungia,*
*Ni wengi wanakujua,*
*kinywaji nichosemea*

*Si wengi nawafumbia,*
*Chai mkifikiria,*
*Chai hii pande mbili,*
*Bayana na tafsida.*

Shairi hili lina kurudia rudia kwa silabi "a" ambayo hufanya vina vya kati na vya mwisho takriri neno.

Mwandishi ametumia pia mbinu ya kurudia neno kwa lengo la kusisitiza jambo fulani Mf. Shairi la "Chai" (Uk.11) ubeti wa sita.

*"Chai naipa haki, kwa kutukidhia haja,*
*Chai imewekwa kati,kwetu sisi sote waja,*
*Chai majani ya miti, hii miti yenye tija,*
*Chai ni mazungumzo, siyo makelele na fujo."*

*"Chai"* *ni* ***takriri neno*** *kwani limerudiwarudiwa kwa kila mstari.*

**Ujenzi wa Taswira**

Mshairi anadhihirisha ufundi wake kwa kuunda picha za mambo mbalimbali katika mawazo ya hadhira yake kwa kutumia maneno. Ameweza kutuchorea picha zinazofanya tuhisi, tuone na hata kunusa au kusikia kilekinachozungumzwa.

Kwa mfano. Shairi la *Tuambae ukasuku (Uk.3):*

> *"Hakuna athubutuye, ati nyati kumtuma,*
> *Aibebe mizigoye au chuchu kumkama,*
> *Na sogi amjaziye, ampandishe kilima,*
> *Nyati si mkubalifu, mfugaji atazikwa."*

Katika ubeti huu tunaona taswira ya kimaumbile. Mwandishi amemchora nyati aliye mkali, mwenye nguvu, mbabe na asiyefugika kujenga picha ya jinsi mtungaji wa mashairi anavyotakiwa kuwa. Anawaasa washairi kuwa wakali na wasiwe waoga katika kueleza ukweli unaokabili jamii.

Katika shairi hilohilo, mwandishi ametumia picha ya farasi walio watumwa wa viongozi. Washairi kama hawa huogopa kusema ukweli kwa sababu ya kuwa vikaragosi vya wale wenye mali na vyeo mbalimbali. Ubeti wa tatu, mstari wa tatu na wa nne mwandishi anasema:

> *" Nchi takumbwa na juto, la watu kuwa farasi.*
> *Farasi yu mtiifu, chanzo cha utumwa wake."*

Kwa upande mwingine, mwandishi anajenga taswira ya kunguru aliye mwoga na akafaulu kuelezea woga walio nao washairi wengi.

Mwandishi pia amejenga taswira ya fimbo ambayo ikishakamatwa haifurukuti tena mpaka mwenye kuikamata auawe. Picha hii inaonyesha utumwa wa washairi wa kuwanyenyekea wakubwa.

Mwandishi katuchorea taswira za hisia kwa mfano katika shairi la *"Kuna nini huko ndan?"* (Uk.4). Mshairi amejenga taswira ya harufu ya kunukia.

Hii inaijengea hadhira hisia za tamaa ya kutamani kitu fulani. Shairi lenyewe linaonyesha tamaa walizo nazo baadhi ya viongozi

ambao mara wapatapo madaraka huwasahau wale waliowapa madaraka.

Hebu tuangalie ubeti huu:

> *"Kuna nini huko ndani,*
> *Mbona jiko lanukia,*
> *Rihi yajaa puani, Na muda wajiendea,*
> *Kisioiva kitu gani,*
> *Mbona mate mwatutoa?*
> *Naona mwajigawia,*
> *Wapishi ni nawahofu".*

Aidha mwandishi amefanya pia taswira za mawazoni katika shauri la "*kimoyo*" (Uk. 12). Mwandishi anaongea na moyo wake. Jambo hili ni la mawazoni tu na haliwezi kutendeka nje ya mawazo. Mfano ubeti wa 1:

> *"Wewe kimoyo sikia, mbona unanipa tabu?*
> *Si mimi, wanionea, kwamba wewe yakusibu,*
> *Ni pole, nakuambia, pole, sina matibabu,*
> *Kimoyo, sinilaumu, uwezo umekuwa haba.*

Mwandishi ametumia pia taswira ya samaki kuashiria baadhi ya viongozi wanaokwepa majukumu kwa kuhofia yaliyo mbele. Hili linajidhihirisha katika shairi la *"samaki kususa chambo" (Uk. 8).*

> *"Kimenishangaza kisa, kilotanda ukumbini,*
> *Samaki chambo kasusa, kukiingiza kinywani,*
> *Ndipo napata hamasa, kuwauliza wendani,*
> *Samaki kasusa chambo, weledi umajinuni"*

Theobald Mvungi pia ametumia taswira ya "*Njiwa*" (Uk.12) kujenga picha ya mpenzi, hususani mpenzi wa kike. Ni kawaida kwa waandishi kutumia picha mbalimbali nzuri akifananisha na mwanamke, kwa mfano ua, njiwa, tausi, malaika; n.k

> *"Mejaribu kujongea, ndege awe mkononi,*
> *Yeye juu hurukia, namwomba sahamani,*
> *Nyimbo ananiimbia, nyimbo za choma moyoni,*
> *Basi miye taabani, njiwa akitabasamu."*

**Kufanikiwa au Kutofanikiwa kwa Mwandishi**
Theobald Mvungi amefanikiwa kusawiri mambo mbalimbali yanayokabili jamii, kisiasa, kiuchumi na kijamii. Aidha, amefanikiwa.

**Kifani kwa upande wa mashairi**
Amezitumia vema kanuni za mtindo wa kimapokeo. Hata hivyo, ameshindwa kwa kiasi fulani kifani katika utunzi wake wa tenzi. Tenzi zake zimekosa sifa ya urefu kama ilivyo ada kwa tenzi. Zina beti chache sana. Mfano utenzi wake wa "Indira" (Uk.18) una beti 8, utenzi wa "utu umekuwa kima" (Uk.19) una beti 5 na kadhalika.

## 12.1.8 ZOEZI LA PILI

*Jibu maswali yafuatayo kisha linganisha majibu yako na yale yaliyotolewa katika kijitabu hiki.*

1. "Shairi kuitwa shairi la kimapokeo huwa limekidhi kanuni fulanifulani. Taja kanuni hizo na jinsi zilivyojitokeza katika kitabu cha *Mashairi ya Chekacheka.*

2. Chagua na kufafanua taswira tatu na kama zilivyotumiwa na Theobald Mvungi katika diwani yake ya *Mashairi ya Chekacheka.*

3. Taja vipengele mbalimbali vya lugha kama vilivyojibainisha katika *Mashairi ya Chekacheka.*

## 12.1.9 MUHTASARI WA SEHEMU YA PILI

Ndugu mwanafunzi, baada ya kuangalia vipengele mbalimbali viundavyo fani, ambacho ni kipengele pacha na maudhui, hebu tujikumbushe tena vipengele hivyo kwa ufupi.

Tumeelezwa uhusiano uliopo kati ya fani na maudhui kuwa hakuna fani bila maudhui. Aidha, hakuna maudhui bila fani. Sasa tuendelee kuiangalia fani kwa ufupi. Tumejifunza kuwa fani katika kazi ya fasihi (Ushairi) huundwa na vipengele vifuatavyo:-

**Muundo**
Tumeona kuwa Theobald Mvungi ameiwasilisha kazi yake ya ushairi kwa kutumia mashairi na tenzi. Kuna jumla ya Mashairi ishirini na saba na tenzi nne. Hakuyawasilisha kinamba wala kimakundi kulingana na maudhui. Mengi ya mashairi yake yapo katika muundo wa tarbia: mistari minne.

**Mtindo**
Mshairi ametumia mtindo mkongwe wa uandishi wa mashairi unaotii kanuni za urari wa vina na mizani: mtindo wa kimapokeo.

**Matumizi ya lugha**
Mtunzi wa *Mashairi ya Chekacheka* ametumia lugha ya kishairi inayojibainisha kwa matumizi ya lugha ya mkato, hata kudondosha baadhi ya herufi ili kupata idadi sawa ya mizani.

Aidha, katika kipengele cha matumizi ya lugha, ametumia:- msamiati, misemo, tamathali za semi kama ifuatavyo:- tashbiha, sitiari, tashihisi, tashititi, takriri na takriri vina.

Mshairi pia ametumia kipengele cha ujenzi wa taswira katika kuiwasilisha kazi yake.

Hatimaye, katika kipengele cha kufaulu au kutokufaulu kwa mwandishi, tumeona kwamba mtunzi amefanikiwa kusawiri mambo mbalimbali yanayoikabili; jamii:- kisiasa, kiuchumi na kijamii kiutamaduni.

Aidha, kwa upande wa fani amefanikiwa sana hasa katika mashairi kwani amemudu kutumia kanuni za mtindo wa kimapokeo. Hata hivyo hakufanikiwa katika utenzi kwani tenzi zake ni fupi ambapo si kawaida ya tenzi.

## 12.1.10 MASWALI YA KUTUMA KWA MKUFUNZI

*Jibu maswali yafuatayo kwenye kitabu cha mazoezi ulichopewa kisha kitume kwa Mkufunzi kwa masahihisho.*

1. Jadili mbinu za kifani zinazojenga kitabu cha *Mashairi ya Chekacheka.* **[Alama 20]**

2. "Ushairi wa Kiswahili kama zilivyo tanzu nyingine za fasihi una kazi ya kuadilisha, kuadibisha na kuelimisha jamii inayoandikiwa" kwa kutumia *Mashairi ya Chekacheka.* Jadili usemi huu. **[Alama 20]**

3. Jadili dhamira ya siasa kama inavyojitokeza katika *Mashairi ya Chekacheka.* **[Alama 20]**

4. Jadili muundo wa kazi ya *Mashairi ya Chekacheka.* **[Alama 20]**

5. "Lugha ya ushairi hujengwa kwa picha na taswira." Thibitisha kauli hii kwa kutumia *Mashairi ya Chekacheka.* **[Alama 20]**

## 12.1.11 MUHTASARI WA SOMO LOTE

Katika somo hili tumechambua vipengee vya fani na maudhui kama vilivyotumiwa na mwandishi wa *Mashairi ya Chekacheka.*

Katika maudhui tumebaini vipengee vya dhamira na ujumbe tuupatao kutokana na kusoma kitabu hicho. Tumejifunza kuwa miongoni mwa dhamira zilizochomoza ni pamoja na kusema ukweli, masuala mbalimbali kuhusu siasa; kwa mfano, mfumo wa siasa wa chama kimoja, demokrasi, suala la kutetea haki, ufujaji wa mali ya umma; uzembe, ukasuku, ulanguzi, mapenzi, dini, dhuluma na majonzi.

Kwa upande wa ujumbe, tumejifunza kuwa:

- Daima tuwe jasiri katika kusema ukweli;
- Viongozi wawajibike ili kuiondolea jamii adha zinazoisonga;
- Tuepuke kuwa kasuku, kukariri na kuhubiri mambo ya majukwaani bila kupima uzito wa yasemwayo;
- Viongozi wa dini waepuke tamaa ya pesa badala yake wahubiri neno la mungu na maadili yake;
- Tuepuke ubadhilifu wa mali ya umma yaani tusitumie nafasi tulizopewa kwa manufaa yetu binafsi;
- Mapenzi ya pesa ni hatari katika jamii. Hivyo, tuepuke kumpenda mtu kwa kujali hali yake kiuchumi. Aidha, kuna ujumbe kuwa ni lazima iwepo ridhaa ya wenzi wote wawili katika mapenzi;
- Ni vizuri kuwaenzi marehemu waliotutangulia kwa yale mema waliyoyafanya enzi za uhai wao;

Kwa upande wa fani tumejifunza kuwa mwandishi wa *Mashairi ya Chekacheka,* ameshadidia mashairi ya kimapokeo, kwani mashairi yake yana urari wa vina na mizani. Aidha mashairi yake ni yale ya mtindo wa tarbia. Pia ametunga tenzi chache katika kazi hii, ambazo pia ni za mtindo wa kimapokeo.

Theobald Mvungi ameonyesha umahiri wake wa kutumia vema lugha ya ushairi ikiwa ni pamoja na lugha ya mkato na iliyosheheni picha na taswira mbalimbali. Aidha, ameipamba kazi yake kwa misamiati, misemo na tamathali mbalimbali za semi.

Hivyo, tunaweza kuhitimisha kwa kusema kuwa mwandishi amefanikiwa kifani na kimaudhui pamoja na kuwa na kasoro ndogondogo kama zile za ufupi wa beti za tenzi.

## 12.1.12 MAJIBU YA MAZOEZI

**Zoezi la Kwanza**

1. Dhamira
   - (i) Kusema ukweli
   - (ii) Majonzi
   - (iii) Dhuluma
   - (iv) Dini
   - (v) Mapenzi
   - (vi) Ulanguzi
   - (vii) Ukasuku
   - (viii) Siasa.

2. Ujumbe/mafunzo
   - (i) Tuwe jasiri katika kusema ukweli.
   - (ii) Viongozi wawajibike ili kuiondolea jamii adha zilizopo.
   - (iii) Tuepuke ukasuku, kukariri na kuhubiri mambo ya majukwaani bila kupima uzito wake.
   - (iv) Viongozi wa dini waepuke tama ya pesa badala yake wahubiri neno la Mungu na maadili mengine
   - (v) Tuepuke ubadhirifu wa mali ya umama, tusitumie nafasi tulizopewa kwa manufaa yetu binafsi.
   - (vi) Mapenzi ya pesa ni hatari katika jamii, hivyo tuepuke kumpenda mtu kwa kujali hali yake kiuchumi.
   - (vii) Ni vizuri kuwaenzi marehemu kwa mema waliyoyatenda wakati wa uhai wao.

**Zoezi la Pili**

1. Urari wa Vina na mizani
   - (i) Matumizi ya mizani 16 kwa kila mshororo.
   - (ii) Matumizi ya vina vya kati na mwisho
   - (iii) Idadi ya mistari nayo ni ile inayokidhi kanuni za mashairi ya kimapokeo. Mistari 2-6

2. Taswira 3
   - (a) Katika shairi la "Tuambae Ukasuku" (Uk.3) tunaona taswira ya kimaumbile. Mwandishi amemchora nyati aliye mkali, mwenye nguvu, mbabe na asiyefugika kujenga picha ya jinsi mtungaji wa mashairi anavyotakiwa kuwa. Anawaasa washairi kuacha uoga, na anawataka wawe wakali na waeleze ukweli unaokabili jamii.

(b) Taswira ya fimbo. Mwandishi ametumia taswira ya fimbo ambayo ikishakamatwa haifurukuti tena mpaka aliyeikamata auawe. Picha hii inaonyesha utumwa wa washairi na kuwanyenyekea wakubwa.

(c) Taswira ya harufu ya kunukia katika shairi la "Kuna nini Huko" taswira hii inajengea hadhira hisia za tamaa ya kutamani kitu fulani.

3. Vipengele vya lugha ni kama msamiati, misemo,tamathali za semi, ujenzi wa taswira, n.k. mifano wa msamiati:
   - Kaumu, kuhodhi,
   - Tafrani, Barakala,
   - Kushadidi, rihi na ufakiri

**Tamathali za Semi:**

***Tashbiha***

- Watu sawa na kamasi (Uk.5)
- Mlevi akakolea kama tumbaku ya tozo (Uk.2)
- Mfanowe kama radi (Uk.13)
- Utaliwa kama pumba (Uk.21)
- Mla punje kama kuku (Uk.3)

***Sitiari***

- Nchi wamefanya kuwa kuti (Uk.2)
- -----------maisha ni safari (Uk.13)
- ----------- sisi ni miamba gogo (Uk.5)

***Tashihisi***

- Moyo unaaswa usiwe na jeuri (Uk.13)
- Ulanguzi umeshona suti (Uk.16)
- Njiwa akitabasm (Uk.12)

***Tashtiti***

- Shairi la "Mtoto aso riziki" ni tashititi kwa walioko madarakani.

***Takriri***

- takriri neon mfano 'chai' katika shiri la chai. (Uk.11)

**Misemo**

1. Taifa wamelizika (Uk.2) = taifa wamelihujumu
2. Msilambishwe viatu (Uk.2) = msiburuzwe ovyo
3. Kushika hatamu (Uk.17) = kushika madaraka.

### 12.1.13 MAREJEO

Mvungi Theobald: 1988 *Mashairi ya Chekacheka*, Education Services Centres Ltd, Dar es Salaam.

Nyangwine, N & Kanyuma, S.Y. 2005 *Tahakiki Vitabu Teule vya Fasihi*, Afroplus Industries Ltd, Dar es Salaam.

**SOMO: 12.2**

**UHAKIKI WA MASHAIRI YA DIWANI YA MLOKA**

## YALIYOMO


| | | UKURASA |
|---|---|---|
| 12.2.1 | Utangulizi wa Somo ... ... ... ... ... ... | 30 |
| 12.2.2 | Malengo ya Somo ... ... ... ... ... ... | 31 |
| 12.2.3 | Utangulizi wa Kitabu ... ... ... ... ... ... | 31 |
| 12.2.4 | Sehemu ya Kwanza: Maudhui ... ... ... ... | 32 |
| 12.2.5 | Zoezi la Kwanza ... ... ... ... ... ... | 40 |
| 12.2.6 | Muhtasari wa Sehemu ya Kwanza ... ... ... | 41 |
| 12.2.7 | Sehemu ya Pili: Fani ... ... ... ... ... ... | 42 |
| 12.2.8 | Zoezi la Pili ... ... ... ... ... ... ... | 52 |
| 12.2.9 | Muhtasari wa Sehemu ya Pili ... ... ... ... | 53 |
| 12.2.10 | Maswali ya Kutuma kwa Mkufunzi ... ... ... | 54 |
| 12.2.11 | Muhtasari wa Somo Lote ... ... ... ... ... | 55 |
| 12.2.12 | Majibu ya Mazoezi ... ... ... ... ... ... | 56 |
| 12.2.13 | Faharasa ... ... ... ... ... ... ... | 57 |
| 12.2.14 | Marejeo ... ... ... ... ... ... ... | 57 |

## 12.2 UHAKIKI WA DIWANI YA MLOKA

### 12.2.1 UTANGULIZI WA SOMO

Mpendwa mwanafunzi, katika somo lililopita ulijifunza uhakiki wa ushairi katika kitabu cha *Mashairi ya Chekacheka.*

Sasa unakaribishwa kuendelea na Somo la Pili katika mfululizo wa masomo yaliyo katika moduli ya uchambuzi wa vitabu teule vya ushairi. Katika somo hili utajifunza uhakiki wa kitabu cha *Diwani ya Mloka.* Somo hili litakuwa katika sehemu mbili; katika Sehemu ya Kwanza utajifunza uchambuzi wa vipengele vya maudhui na katika sehemu ya pili utajifunza uchambuzi wa vipengele vya fani.

Ukumbuke kuwa ni vigumu sana kutenganisha fani na maudhui katika kazi za fasihi, kwani vitu hivi viwili vinafungamana na pengine hata kuingiliana . Katika ushairi mawazo makuu ya mtunzi ndiyo huzingatiwa wakati wa kuhakiki ushairi andishi katika kipengele cha maudhui.

Aidha, katika kuihakiki fani ya ushairi vipengele vinavyozingatiwa ni muundo, mtindo matumizi ya lugha na ujenzi wa taswira. Katika muundo wa ushairi utajifunza matumizi ya mizani, vina, mistari, beti na vituo kama vilivyotumiwa na mwandishi.

Mtindo wa mashairi ni wa aina mbili: yapo mashairi ya mtindo wa kimapokeo na aina ya pili ni mashairi ya kisasa. Mashairi ya kimapokeo huzingatia sana matumzi ya vina na mizani wakati yale ya mtindo wa kisasa ya hayazingatii vina na mizani.

Nayo matumizi ya lugha huzingatiwa katika vipengele vya tamathali za semi, methali, misemo, lugha ya mkato, nahau na ujenzi wa taswira.

### 12.2.2 MALENGO

Baada ya kusoma somo hili unatarajiwa kuwa na uwezo wa:-

- Kubainisha na kufafanua dhamira mbalimbali zilizo katika *Diwani ya Mloka;*
- Kubainisha na kufafanua kwa mifano matumizi ya vipengele mbalimbali vya fani katika diwani hii; na
- Kujibu maswali yoyote hasa ya mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne katika somo la fasihi andishi na hasa sehemu ya ushairi.

### 12.2.3 UTANGULIZI WA KITABU

Ndugu Mwanafunzi, neno diwani lina maana ya mkusanyiko wa mashairi, tenzi au mashairi na tenzi zilizotungwa kwa nyakati tofauti na mwandishi mmoja tu. Hatimaye, mashairi yakakusanywa na kuwekwa pamoja na kufanya kitabu.

Diwani ya Mloka ni mkusanyiko wa mashairi na tenzi zilizotungwa na mwandishi Charles Mloka kwa nyakati tofauti tofauti. Mwandishi ameigawa kazi yake katika makundi matatu. Yapo mashairi na tenzi za mawaidha au maadili, mashairi yahusuyo lugha na fasihi na kundi la tatu ni yale yanayohusu siasa na uchumi. Makundi yote haya matatu, yamo mambo mengi yaihusuyo jamii yaliyojadiliwa, kwa mfano maombolezo, utamaduni, umuhimu wa kufanya kazi, mawaidha/maonyo, elimu, siasa, mapenzi na mengineyo.

## 12.2.4 SEHEMU YA KWANZA: MAUDHUI

**Dhamira**

Hebu sasa tuangalie namna gani mwandishi alivyoiumba kazi yake kimaudhui kwa kuangalia masuala mbalimbali aliyoyajadili. Yaani kipengele cha dhamira.

Miongoni mwa dhamira zinazojitokeza katika *Diwani ya Mloka* ni pamoja na:-

**Utamaduni**

Mwandishi anatueleza kuwa mahali popote wanapoishi watu kuna utamaduni. Anaongeza kuwa taifa lisilo na utamaduni ni Taifa lililokufa. Mawazo haya tunayapata katika shairi la utamaduni katika ubeti wa kwanza:

*Palipo na watu hai, hapakosi utamaduni,*
*Hapa ndipo panadai, sanaa za kila fani*
*Aghalabu pana rai, rahisi zetu moyoni*
*Utamaduni sauti ya maisha ya jamii.*

Katika kulifafanua suala la utamaduni mwandishi ameonyesha kuwa kila kabila lina utamaduni wake unaojumuisha lugha, sanaa mbalimbali, vyakula na mavazi.

Vilevile mwandishi anaitukuza lugha ya Kiswahili kutokana na umaarufu wake unaoifanya izidi kukua na kujipatia umaarufu hata sehemu nyingine za dunia. Katika ubeti wa arobaini na moja (Uk.61) wa utenzi mwandishi anasema:

*"Kiswahili hivi sasa,*
*Mepiga hatua hasa,*
*Watu wengi wananata*

*Katika hii dunia"* Na katika ubeti wa arobaini na nne (Uk.61) mwandishi anaonyesha nafasi ya Kiswahili duniani anasema:

*Hadi sasa ni ya sita,*
*Kati ya lugha matata,*
*Zilizopata kupita,*
*Kwenye hadhi ya dunia.*

Aidha, mtunzi ameonyesha kwa ufupi historia ya Kiswahili na asasi zilizojihusisha na kukua na kuenea kwake. Mashairi mengine yanayoiongelea lugha ya kiswahili ni "Kiswahili" (Uk.

50). Shairi hili linatuhimiza kuiendeleza lugha ya kiswahili, kufundishia kiswahili." (Uk.54). Mshairi anatoa wito kwa serikali ione umuhimu wa kuifanya lugha ya Kiswahili kuwa lugha

ya kufundishia shuleni; "alimu wa Kiswahili '(Uk. 51). Katika shairi hili tunaonyeshwa kuwa walimu na wasanii wanao wajibu wa kukiendeleza kiswahili.

**Umuhimu wa Kufanya Kazi**

Hii ni dhamira nyingine inayojitokeza katika diwani hii. Mwandishi anatueleza kuwa binadamu bila kufanya kazi huwa ni kiumbe wa kushangaza. Anamfananisha yule asiyefanya kazi na kuku kwani kuku hana mawazo ya kufanya kazi lakini hupata riziki yake pale binadamu akusanyapo mazao yake. Mawazo haya yanapatikana katika ubeti wa pili katika shairi la "kuku" (Uk.25) mwandishi anaposema:

*"Namshangaa kiumbe, aishiye kama kuku,*
*Nimpe upi ujumbe, naye apate ruzuku,*
*Ulimwengu wenye njaa, na shidaze kama hizi,*
*Haututaki kukaa, pasipokufanya kazi,*
*Nimwoneje mwanadamu, asiyependa kulima."*

*Huku maisha magumu, yangali yamuandama,*
*Aishije duniani, kuku asipomkana,*
*Nimuweke kundi gani, kazi anapoiguna?*
*Neno la mwili kutenda, dunia mtu shughli,*
*Ndilo huleta matunda, yanayobadili hali."*

Aidha, katika kuhimiza kazi mwandishi anatueleza kuwa kila kitu duniani kimetengenezwa kutokana na kufanya kazi. Tunalinganisha methali, "usione vyaelea vimeundwa" na shairi lake la "Usione ukadhani." Mwandishi anawafunza wale wanaodhani kuwa mafanikio yanakuja yenyewe tu bila kufanya kazi; katika ubeti wa tatu wa shairi hilo anasema:

*"Sione mtu kuchuma, ukafikiri kuiba,*
*Sione watu kulima, ukadhani wanashiba,*
*Sione penye huruma, ukahisi pana tiba,*
*Sione pepo kuvuma, ukafikiri dhoruba,*
*Sione panapochoma, ukadhani pana mwiba,*
*Kila unachotazama,usione ukadhani." (Uk.3).*

**Umuhimu wa Elimu**

Ndugu Mwanafunzi,

Suala la elimu limejadiliwa na mwandishi. Katika shairi la "Kujielimisha" (Uk.27) mwandishi anatueleza ubora au umuhimu wa elimu. Anaona kuwa elimu ni chanzo cha kila kitu, bila elimu binadamu hawezi kufanikiwa kwa lolote au kupata maendeleo. Mwandishi anabainisha kuwa ukitaka kupata elimu itakayokusaidia kupata maendeleo au hali bora kimaisha ni lazima utaabike anasema,

*"Neleze utamu gani, elimu uliyonayo,*
*Nieleze vitabu nini, mbele ya elimu hiyo,*
*Nionje wapi hekima, kama sio kwa elimu,*
*Niende wapi kusoma, vitabu nikilaumu,*
*Na waliofanikiwa, wanasahau daima,*

*Sasa unalolipinga na lipi walitegua*
*Wenzetu walikubali, kwanza kuchuma mpunga,*
*Ndipo walikula wali, mchele walipotwanga,*
*Ndege hufika angani, anapotumia mbawa,*
*Lakini hubaki chini, mbawa asipoinuwa." (Ub.2).*

Kwa upande mwingine, mwandishi anaongelea ubora wa elimu kwa maisha yetu kwa kutuonyesha jinsi elimu inavyotuwezesha kujipatia maendeleo kwa kutatua vikwazo vinavyokuwepo. Katika shairi la "Nilipokuwa na Kiza"(Uk. 28) mwandishi anasema:

*"Maisha ni kutazama, wapi ulikotokea,*
*Wapi uliposimama, wapi ulipofikia,*
*Na wapi unapokwenda, katika maisha yako,*
*Kipi ulichokiunda, na kipi hakiko kwako,*
*Lipi unalolipanga, na lipi walitegua."*

*Nini kinachokutinga na vipi nakitatua,*
*Kuendelea kwa mtu, hutegemea akili,*
*Jinsi inavyothubutu, kupambana nayo hali,*
*Hayawi maendeleo, bila mtu kufikiri*
*Hayaji maendeleo, bila tabu kudhihiri*
*Palipo kuwa na shida, ndipo huchemshwa bongo." (Ub.2).*

**Nafasi ya Mwanamke**

Miongoni mwa masuala yaliyoishughulisha akili ya mwandishi ni ukombozi na nafasi ya mwanamke katika jamii. Katika shairi lake la "Uhuru" (Uk.18), mwandishi anaitaka jamii impe uhuru mwanamke ili naye aweze kutoa mchango wake katika shughuli

mbalimbali za maendeleo katika jamii badala ya kukaa jikoni tu. Tunasoma:

*"Uhuru wa mwanamke, kuonja mboga jikoni,*
*Hapo akibaki peke, mapishi huyakafini,*
*Na akija mume wake, haoni kitu kigeni,*
*Palipo na hindi teke, na suke huko shambani,*
*Haifai ulishike, kila mara mkononi,*
*Liache nuru liweke, utalila kwa amani,*
*Hunenepa chungu chungu, shimoni akiwa huru." (Ub.3)*

**Mapenzi**

Dhamira nyingine iliyojitokeza katika *Diwani ya Mloka* ni suala la mapenzi. Mwandishi anaonyesha hali ya majonzi yajitokezayo miongoni wa wapenzi pale inapotokea wapenzi hao kuachana.

Katika shairi lake la "Chozi lishikalo moyo" (Uk.23) mwandishi anafafanua adha zimpatazo yeyote anayekuwa ametengana na aliyempenda kwa dhati. Katika ubeti wa pili anasema:

*"Haliwi kulikausha,japo pawepo kausho,*
*Haliwi la kulivusha, liishe leo na kesho,*
*Chozi hili la maisha, uchungu wake tabisho,*
*Humtenda mtu kwisha, bila kutambua mwisho,*
*Daima humkondesha, sipopata suluhisho,*
*Chozi lishikalo moyo, vigumu kulikausha."(Ub.2)*

Akizidi kulijadili suala hili la mapenzi, mwandishi anaonya kuhusu utoaji wa sifa. Katika shairi la "Sifa na Kashfa" (Uk.16) fanani anatueleza kuwa sifa ni motisha chanya na kashfa ni motisha hasi kwa wapendanao. Anaeleza kuwa mpenzi wako ukimpa sifa hufurahika sana na wapenzi wawili wataelewana lakini kama kuna kashfa basi italeta uhasama katika mapenzi. Kashfa ya kumsema mtu, kumsengenya; n.k. huharibu mahusiano ya kimapenzi. Mwandishi anahitimisha ubeti wa kwanza kwa kusema, "sifa ni motisha chanya, kwa kila wake mpenzi" na katika ubeti wa pili "kashfa motisha hasi, kwa kila wake mpenzi".

Shairi jingine linaloongelea suala hili ni "Hutaniacha Morogoro I na II (Uk. 41 - 42). Katika shairi hili msanii anaonyesha madhara yanayotokea pindi wawili wapendanao wanapoachana kwa muda hata kama mmoja wao anasafiri, majonzi na huzuni ni jambo la kawaida kwa wapendanao.

**Maadili Mema na Maonyo**

Mwandishi wa diwani hii ameonekana mwadilifu kwa kuiandikia jamii mashairi yanayotoa maadili na maonyo kuhusu maisha yetu ya kila siku. Kwa mfano ametumia shairi la "Ubinafsi" (Uk. 13) kuonyesha tabia mbaya ya binadamu kuwa na ubinafsi. Anaikemea tabia hiyo na kusema ubinafsi unasababisha choyo, chuki, maringo, na tamaa mbaya. Anasema:

"......................................................
*Palipo na ubinafsi, hapakosi kuwa choyo,*
*Na upeke wa nafsi, na chuki katika moyo,*
*Haukosekani wivu, maringo pia tamaa,*
*Kadhalika na ubavu, wa moyo usiofaa,*
*Ni tabia ya asili, mtu ana ubinafsi,*
......................................................"

Shairi jingine lenye kuadilisha ni "Fitina" (Uk.14). Hapa mwandishi anakemea tabia ya watu kuwafitini wenzao. Aidha anatahadharisha kuwa fitina inapozidi inaleta uadui.

Kama vile haitoshi, mwandishi anazidi kuionya jamii kuhusu suala la kuwatafuta wabaya kutoka mbali. Yeye anaamini kuwa "kikulacho kinguoni mwako", hii inadhihirika katika shairi lake la "chawa aliyekichwani" (Uk.15). Anaeleza kuwa adui yako ni yule aliye karibu nawe, anaweza kuwa ndugu au rafiki yako.

Vilevile, mwandishi anakemea tabia ya baadhi ya wenye nyumba za kupanga kuwanyanyasa wapangaji wao kwa kuwawekea sheria mbalimbali. Katika shairi lake la "Simba kukaa na nyani" (Uk.16) mwandishi anaonyesha kuwa wapangaji wengi huamua hata kuishi katika nyumba zisizofaa ilimradi tu hakuna bugudha ya wenye nyumba. Anasema:

*"Naishi katika gofu, kuhama sina satua,*
*chumba hakina sakafu, ya kuweza kuvutia,*
*Nakaa kwa takilifu, kutwa nikifua pua,*
*Na panya wenye minofu, nimechoka kuwaua,"*

*"Hata hivyo sijadhofu, kwa kubambwa na sheria,*
*Nina uhuru sufufu, wa kutenda kwa tabia.*
*Japo watu wakashifu, nyumba nimeng'ang'ania,*
*Haijanipata hofu, ya kutaka kukimbia,*
*Simba kukaa na nyani, mtini wataumana." (Ub.3).*

Mwisho, mwandishi anaadilisha jamii kuwa ingawa elimu ni kitu bora, bado hekima ni bora zaidi hasa kama mwenye elimu hana

busara kwani huwa hathaminiki. Anaonyesha kuwa mwenye elimu na hekima huwa ni bora na anafaa kwa uongozi katika jamii. Mawazo haya yanatolewa katika shairi la "Hekima bora zaidi" (Uk.34), tunaambiwa:

*"Elimu bila hekima , ni mtu kukosa jina,*
*Hekima ndiyo heshima, ya elimu ikafana,*
*Hii ndiyo sifa njema, hata ukisoma sana,*
*Ingawa elimu bora, hekima bora zaidi." (Ub.3).*

**Maombolezo**
Katika dhamira hii ya maombolezo mwandishi ametumia "utenzi wa hayati Sokoine"(Uk.68) kueleza kifo cha aliyekuwa waziri mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1984) Hayati Edward Moringe Sokoine na jinsi kifo hicho kilivyotokea na kupokelewa kwa majonzi na wananchi. Mwandishi anasema,

*"Kwa sauti ya majonzi,*
*Mwalimu kashusha Pumzi,*
*Kutujulisha mpenzi,*
*Sokoine katufia." (Ub.3)*

*"Wengi walimlilia,*
*Vile wakimwangalia,*
*Kama amejilalia,*
*Na hata wakazimia." (Ub.26).*

**Kuinua Uchumi**
Suala la uchumi nalo limejadiliwa sana na mwandishi akitoa rai ya kuwa ili tuweze kujikomboa kiuchumi ni lazima kutumia aridhi tuliyonayo kwa manufaa zaidi ili kuondokana na umaskini wetu. Katika shairi lake la "Ardhi Ujitazame" (Uk.21) mwandishi anasema:

*"Jembe nimeshajinoa, ardhi kukuondoa,*
*sinione nimepoa, ningali nakudondoa,*
*nangoja kujikomboa, nitapovuka mikoa,*
*mahindi nimeopoa,nimebaka kukoboa,*
*ghamidha nitaitoa aridhi, nikikunyoa.*
*Jembe ninaporejea, ardhi ujitazame." (Ub.4)*

Aidha, mwandishi anaielimisha jamii kuwa ili kuweza kufanikiwa ni lazima kuvumilia tabu pale tunapokuwa tumedhamiria kupata mafanikio katika jambo fulani. Anaonyesha kuwa "baada ya dhiki faraja." Hivyo watu wasikatishwe tamaa na vikwazo wakutanavyo

navyo katika harakati zao za kujikomboa. Katika shairi la "Baada ya jua kali." (Uk. 29) anasema:

*"Liwakapo kwa marefu, jua huzaa mateso,*
*Yawezayo kusarifu, adha za kila mnuso,*
*Viumbe hukimbia, huliona ni adui,*
*Lakini mvumilie, mbeleni hulinywa tui,*
*Linapofunguka wingu, hutulia mwanadamu."* (Ub.2).

Vilevile, katika shairi la "Matatizo si kushindwa" (Uk.85) mwandishi anaonyesha kuwa kutokuwa na nafasi nzuri kiuchumi si kwamba tumeshindwa kuyatatua matatizo tuliyo nayo bali vipo vikwazo toka nje vinavyosababisha tuendelee kukwama katika harakati zetu za kujikomboa. Mwandishi anatoa mifano ya maelekezo yatolewayo na benki ya dunia na shirika la fedha na jinsi tusivyoweza kujikwamua kutokana nayo. Katika ubeti wa sita mwandishi anasema:

*"Lakini kasisitiza, sababu kutoka nje,*
*Ndiyo hasa zatufanza, matumizi, tuyachinje,*
*Hususani tukiziuza, bidhaa nchi za nje,*
*Kuwepo kwa matatizo, si dalili ya kushindwa."*

Zaidi ya hayo, mwandishi anasisitiza juhudi katika kila sekta ili kuinua uchumi. Anasisitiza ushirikiano katika mashamba, viwandani na kila mmoja katika nafasi yake ashiriki vema ili uchumi wetu usonge mbele. Haya mawazo tunayapata katika shairi la "Nasaha za mwaka Mpya" (Uk.87) Katika ubeti wa 29 anasema:

*"Wenyeviti wa vijiji, umoja udumisheni,*
*ufikapo ulimaji, nyote mwende shambani,*
*kuinua mahitaji, tunayotaka nchini,*
*mwaka mpya umefika, tuuinue uchumi."*

Akiwahimiza wafanyakazi wa viwanda na anasema:

*"Na sisi kwenye viwanda, tuzalishe mali sana,*
*Tuhakikishe twaunda, vitu vingi kwa kuvuna,*
*Huku kazi tukitenda, kwa nguvu zenye kufana*
*Mwaka mpya umefika, tuinue uchumi."* (Ub.30).

Kitu kingine alichokiongelea mwandishi ni suala la ulanguzi na uhujumu uchumi. Anatoa ari kwa wananchi kuhakikisha kuwa tunapiga vita vitendo vyote vinavyorudisha nyuma harakati zetu za kuinua uchumi. Katika "Utenzi wa Hayati Sokoine;" mwandishi

anatushauri kuyaenzi yale mazuri aliyokuwa ameyaanzisha. Anasema:

*"Pamoja na wahujumu*
*Hakupenda wadhulumu,*
*Mali hii ya kaumu,*
*Vita kuwafungulia."* (Ub.63)

Mpendwa mwanafunzi, *Diwani ya Mloka* ni kitabu kilicho na masuala mengi sana yanayoihusu jamii yetu. Haya tuliyoyachambua ni machache tu miongoni mwa yale yaliyojadiliwa na mwandishi. Hivyo, usichukulie kuwa haya ndiyo masuala pekee yaelezwayo na mwandishi. Aidha, usishagae kuwa shairi moja linaweza kuongelea zaidi ya suala moja. Hii ndiyo kazi ya fasihi, ya kumgusa mwanadamu kulingana na mazingira anamoishi.

**Ujumbe**

Baada ya kujifunza dhamira zilizomo katika *Diwani ya Mloka*, hebu sasa tuangalie ni ujumbe gani tuupatao kutoka katika kazi hii. Kwa kupitia dhamira mbalimbali tunapata ujumbe kama ifuatavyo:

Kwanza, ubinafsi, fitina, sifa mbaya na kashfa ni chanzo cha chuki, choyo, wivu, na tamaa mbaya katika jamii. Hivyo, tuviepuke ili kuweza kujenga jamii yetu.

Pili, elimu ni ufunguo wa maisha. Hivyo, ni wajibu wa kila mwanajamii kujielimisha na kutumia elimu yake kwa busara.

Tatu, mtu mwenye hekima ni wa muhimu sana katika jamii kwani atatumia hekima yake kuelimisha umma kuhusu mema na mabaya yaliyopo katika jamii.

Nne, ili kuinua uchumi wetu hatuna budi tufanye kazi kwa bidii, tuondokane na ulanguzi na uhujumu uchumi.

Tano, ili kujikomboa kiutamaduni ni lazima tudumishe utamaduni wetu ikiwemo lugha yetu ya kiswahili.

Mwisho, ni vigumu kusahau uhusiano uliopo baina yako na mtu umpendaye kwa dhati. Hii ni kutokana na kwamba mawazo yako yote huwa daima juu yake.

### 12.2.5 ZOEZI LA KWANZA

*Jibu maswali yafuatayo kisha linganisha majibu yako na yale yaliyotolewa katika kijitabu hiki.*

(1) Ni dhamira zipi zinajadiliwa katika Diwani ya Mloka? (Taja dhamira tano tu).

(2) Eleza maana ya Diwani?

(3) Taja maadili manne tuyapatayo kwa kusoma *Diwani ya Mloka.*

(4) Mashairi ya *Diwani ya Mloka* yamepangwa kimaudhui katika makundi matatu. Yataje.

## 12.2.6 MUHTASARI WA SEHEMU YA KWANZA

Ndugu Mwanafunzi, katika sehemu hii tumejifunza masula mbalimbali katika *Diwani ya Mloka*. Kwa ufupi, masuala hayo yamepangwa katika makundi matatu: yapo ya kimaadili na mawaidha, yahusuyo lugha na fasihi na hatimaye masuala ya siasa na uchumi. Katika kila kundi yamejadiliwa masula kadhaa. Kwa mfano, kwenye maadili na mawaidha mwandishi anakemea ubinafsi, fitina, sifa na kashfa. Katika lugha na fasihi mwandishi anasisitiza umuhimu wa kuendelea kukikuza Kiswahili. Aidha, katika siasa na uchumi anakemea suala la matabaka, kutotenda haki na kusisitiza kuhusu suala la kuinua uchumi.

Aidha, ujumbe tuupatao kwa kusoma diwani hii umejikita sana katika dhamira zilizoibuliwa katika mashairi. Mwandishi wa *Diwani ya Mloka* anatuambia kuwa ubinafsi, fitina na mambo mengine kama hayo hujenga tabia mbaya katika jamii. Pia, anaonyesha umuhimu wa kufanya kazi ili kuinua uchumi, umuhimu wa elimu na matumizi yake; kwani anaona kuwa hekima ni kitu bora zaidi ya elimu hivyo anatuelimisha kuwa na busara hata kama tukiwa na kisomo. Vilevile, mwandishi anaitaka jamii kudumisha utamaduni, ikiwemo lugha ya Kiswahili. Mwisho, ni vigumu kuusahau uhusiano uliopo baina ya mwenzi wako hata mkiachana kwa muda.

## 12.2.7 SEHEMU YA PILI: FANI

Mpendwa mwanafunzi, sasa umemaliza sehemu ya kwanza ya uchambuzi wa *Diwani ya Mloka* ambayo ni Maudhui Bila shaka umefurahia somo na umetalii kwa makini vipengele vinavyounda maudhui. Sasa unakaribishwa katika sehemu ya pili ya uchambuzi ambayo ni fani. Tunakusihi uwe makini ili uvielewe vipengele hivi na jinsi vilivyotumiwa na mwandishi Charles Mloka.

Malengo ya sehemu hii ni kukuwezesha:

- kutaja na kufafanua muundo na mtindo aliotumia mwandishi;
- kutaja na kutoa mifano kwa kila kipengele cha matumizi ya lugha;
- kueleza, kufanana au kutofautiana kwa fani kati ya kazi za ushairi na zile ambazo si za ushauri.

Kabla ya kuanza kuchambua hebu tujikumbushe maana ya fani. Fani ni ufundi au ustadi anaoutumia mshairi katika kazi yake. Fani ya kazi ya fasihi hutofautiana toka utanzu mmoja hadi mwingine. Hivyo, kipengele hiki hujumuisha muundo, mtindo na matumizi ya lugha.

**Muundo**

Kabla ya kuangalia muundo wa *Diwani ya Mloka*, hebu tujiulize, je muundo ni nini? Swali hili si geni kwako kwani toka mwanzo tumekuwa tukijikumbusha fasili ya muundo. Muundo ni namna kazi ya fasihi ilivyopangwa au ilivyojengwa. Tujiulize tena, je, mwandishi Charles Mloka ametumia muundo gani? Katika kuangalia muundo wa *Diwani ya Mloka* tutaangalia beti, mstari, mizani, vina, na kituo. Katika mashairi, shairi lenye beti chache ni shairi lenye beti mbili, mfano shairi la "kuku" (Uk.25), "*Jua halitoki chini*" (Uk.22), *Kujielimisha* (Uk.27) na shairi refu lina beti thelathini na nne. Mfano ni shairi la "Nasaha za Mwaka Mpya (Uk.87). Katika tenzi, utenzi mfupi una beti ishirini na moja na utenzi mrefu una beti mia moja na nne. Mfano "Utenzi wa hayati Sokine" (Uk.68). Mistari kwa kila ubeti kama mashairi ya mtindo wa kimapokeo ni mistari minne (tarbia) hadi sita (tasdisa). Mifano ya mashairi ya mistari sita ni:

*Jua halitoki chini* (Uk.21)
*Chozi lishikalo moyo* (Uk.22)

*Jembe likilimia ukumbini hukongoka* (Uk.24)
*Usione ukadhani (Uk.26)*
*Hutaniacha Morogoro shairi la I na II* (Uk.41-42)
*Mawe ya kale* (Uk.81)
*Kiswahili* (Uk.50).

Mifano ya mashairi yenye mistari minne (tarbia) ni kama ifuatavyo:

*Waandishi wa habari* (Uk.32)
*Kufundisha Kiswahili* (Uk.54)
*Nyoka amemgonga mbuzi* (Uk.77)
*Chokochoko ya haki* (Uk.79)
*Nasaha za Mwaka mpya* (Uk.87)
*Wito wake mwenyekiti* (Uk.83)

*Mizani*

Mizani kwa kila mistari ni 16 mfano katika shairi la "*utamaduni*" (Uk. wa 47).

| "Pa | li | po | na | wa | tu | ha | i | ha | pa | ko | si | ta | ma | du | ni" |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 |

Katika tenzi kuna mizani nane kwa kila mstari. Mfano, utenzi wa Hayati Sokoine (Uk.68).

*Ilikuwa redioni*
*Saa kumi za jioni*
*Mwenyekiti kwa huzuni*
*Umma akautangazia*

*Tarehe kumi na mbili*
*Ya mwezi wa Aprili*
*Themanine kamili*
*Msiba ulitokea*

Aidha, katika beti kuna baadhi ya mistari ambayo haina mizani 16. Mistari hii ni michache sana. Mfano, mstari wa kwanza (Ub.2) katika shairi la "Mtu aliyefikiri" (Uk.20).

"$\frac{ma}{1}$, $\frac{i}{2}$, $\frac{sha}{3}$, $\frac{mwa}{4}$, $\frac{na}{5}$, $\frac{da}{6}$, $\frac{mu,}{7}$, $\frac{ni}{8}$, $\frac{sa}{9}$, $\frac{wa}{9}$, $\frac{sa}{11}$, $\frac{wa}{12}$, $\frac{na}{13}$, $\frac{ga}{14}$, $\frac{ri.}{15}$" Msitari una mizani 15

*Vina*

Katika mashairi ya *Diwani ya Mloka* kuna vina vya kati na vya mwisho kwa mistari mitatu ya mwanzo katika beti isipokuwa mstari wa mwisho ambao hutofautiana na mistari mingine. Mfano katika shairi la 'Alimu wa Kiswahili' (Ub. 3, Uk. 51).

*Hii yaonyesha fika washairi ni muhimu,*
*Tena inayumkika, tuwaite ni walimu,*
*Wawezao kumulika, wenzi wao binadamu,*
*Ulimi mtoa neno, hifadhi kinywa vizuri.*

Aidha, kuna wakati anabadilisha silabi (vina) vya kati kila baada ya mistari kadhaa. Utumizi huu hauna kanuni kwani kwingine anafanya hivyo kila baada ya mistari 2 na kwingine hubadili baada ya mistari 4; n.k. mfano, shairi la "*Mwanadamu na maisha*" (Uk.30, Ub.3):

"*Naamini vipi nishuku, maishani iko siku,*
*Mola ataikhuluku, nipate yangu ruzuku,*
*Naaminije Mungu yupo, huku matatizo yapo,*
*Nioneje wapi nipo, Imani ikiwa hapo,*
*Kama siyo kunijia, mawazo ya utopia,*
*Nini kitafuatia, ikiwa nazingatia.*"

Angalia mfano mwingine katika shairi la Baada ya jua kali. (Uk.29, Ub.1).

"*Baada ya jua kali, mvua kubwa itanyesha.*
*Kwa yule ambaye mwili, ulikuwa unakwisha,*
*Mithili yake kaburi, litembealo daima,*
*Na sanda ya ufakiri, mwilini uliosimama,*
*Kunyesha huko kwa mvua kutaangusha madafu.*"

"*Kaburi litachukua, na kuyanywa bila hofu,*
*Matunda ya adha nyingi, siku hiyo yatashuka,*
*Mbele yao watu wengi, yatakuwa kama duka,*
*Wengine watanunua, wakikumbuka kaburi.*
*Lilivyopiga hatua, katikati ya sayari.*"

Baada ya kuona muundo aliotumia mwandishi, sasa tuangalie mtindo.

**Mtindo**

Mtindo wa mashairi ni wa aina mbili, aina ya kwanza ni mashairi ya kimapokeo, yaani mashairi yanayofuata urari wa vina na

mizani, beti, mistari; n.k. Aidha, mashairi ya usasa hujulikana pia kama masivina/mapingiti, ukwafi.

Mfano wa mashairi yenye mtindo wa kimapokeo ni: "Utamaduni" (Uk.47), "Kiswahili" (Uk.50), "Chokochoko ya Haki" (Uk.79), "Samaki wamekasirika" (Uk.78), "Wito wake Mwenyekiti" (Uk.83), "Nasaha za Mwaka Mpya" (Uk.87).

Mfano wa mashairi yenye mtindo wa usasa ni: "Ubinafsi" (Uk.13), "Fitina" (Uk.14), "Chawa aliye kichwani" (Uk.15), "Simba kukaa na Nyani" (Uk.16), "Kifungo" (Uk.19), "Mtu aliyefikiri" (Uk.20), na kadhalika.

Aidha, mwandishi ametumia mtindo pekee pale alipoyagawa mashairi yake kulingana na dhamira. Ameyagawa mashairi yake katika sehemu tatu. Sehemu ya Kwanza ni ile inayobeba mashairi ya mawaidha/maadili; Sehemu ya Pili ni mashairi ya lugha/fasihi na sehemu ya tatu ni ya mashairi ya siasa/uchumi. Mtindo huu unampa upekee na kumtofautisha na waandishi wengine.

**Matumizi ya Lugha**
Kipengele kingine katika fani ni matumizi ya lugha. Hapa tunaangalia vionjo mbalimbali vilivyotumiwa na mwandishi ili kuipamba kazi na kuipa mvuto.

Mshairi ametumia lugha nyepesi ambayo msomaji anaweza kuielewa vizuri na kupata ujumbe mara asomapo. Aidha, ametumia lugha ngumu kwa baadhi ya mashairi. Pia, mshairi ametumia lugha ya mafumbo, hasa kwa yale yaliyotumia lugha ngumu, yenye picha na taswira. Mfano shairi la Nyoka Amemgonga Mbuzi. (Uk.77).

Kwa sura ya nje nyoka na mbuzi vyote vinafahamika kwa wasomaji lakini picha na taswira zinazoletwa na wanyama hao ni tofauti. Mbuzi anawakilisha viongozi au tabaka la wanaotetea wanyonge (tabaka la chini).

Siafu katika ubeti anaonyesha picha ya tabaka la wanyonge au raia wa nchi. Picha nyingine ni ile ya samaki wamekasirika (Uk.78), "Mawe ya kale" (Uk.81). Ufafanuzi wa taswira zinazojengwa na picha utatolewa katika kipengele cha taswira.

Hayo ni baadhi ya mashairi ambayo ametumia lugha ngumu ya picha na taswira na hivyo kumfanya msomaji asielewe ni nini mshairi anachozungumzia, ingawa picha hizo zinafahamika.

Mbinu nyingine alizotumia mshairi ili kuipamba lugha yake ni tamathali mbalimbali za semi. Tamathali hizo zitafafanuliwa kulingana na aina zake

**(a) Tashbiha:**

Ulinganifu wa vitu viwili kwa kutumia viunganishi kama vile, kama, mithili ya sawa na; na kadhalika.

(i) Wamepangwa kama kuni (shairi la nyoka amegonga mbuzi (Uk.77) mstari wa I (Ub.1).

(ii) Aliweza kujificha kama nyenyele shimoni (shairi la "Mawe ya Kale" (Uk.81, Ub.1, mstari wa 1).

(iii) Na nguoni hujibana, mkame kama nyenyele (Shairi la "Chawa Aliye Kichwani" (Ub.2, mstari wa 8).

(iv) Dunia ni kama wavu, majini unaotembea. (Shairi la Kifungo (Uk.19, Ub.2 mstari wa 1).

(v) Haliwi kama sikio, linapopata zibuo (shairi la Ardhi Ujitazame (Uk.21, Ub.3, mstari wa 3 na 4).

(vi) Haliwi la tumainio kama chai kwa chujio "Shairi la Ardhi Ujitazame" (Uk. 21, Ub. 3, mstari wa 3 na 4).

(vii) Viumbe kama ndege "Shairi la Ubinafsi" (Uk.13, Ub.2, mstari wa 3).

(viii) Mithili yake kaburi "Baada ya Jua Kali" (Uk.29, Ub.1).

(ix) Uhuru moyoni mwako ni kama nuru ya mwezi. "Uhuru" (Uk.18, Ub. 2, mstari 1).

(x) Ninamshangaa kiumbe aishiye kama kuku "Kuku" (Uk.25, Ub.2, mstari 1).

(xi) Kiswahili lugha tamu kama maji ya mtungi "Kiswahili" (Uk.50, Ub.1, mstari wa1).

**(b) Sitiari:**

Ulinganifu wa vitu viwili pasipo kutumia viunganishi.

(i) Kazini ni darasani shairi la "Fitina" (Uk.14, Ub.1, mstari wa 1).

(ii) Chawa ni huyo kinyozi mtia wembe kichwani shairi la "Chawa Aliye Kichwani" (Uk.15, Ub.1).

(iii) Fitina titi la paka halifai kwa mtindi "Fitina" (Uk.14, Ub.1, mstari wa mwisho).

(iv) Fitina ngozi ya tembo haifai kwa kuwamba shairi la "Fitina" (Uk.14, Ub.2 - 3, mistari ya mwisho).

**(c) Tashihisi:**

Vitu visivyo na uwezo wa kutenda kama binadamu vinapewa uwezo huo.

(i) Wameshikwa na hamaki, wakimbilia sokoni shairi ni hilo hilo la "Samaki wamekasirika" (Uk.78).

(ii) Nyoka mshika risasi "Nyoka Amegonga Mbuzi" (Uk.77, Ub.1, mstari wa 2).

(iii) "Jembe Nitaporejea Ardhi Ujitazame" (Uk.21) kwa kila mstari wa mwisho wa kila ubeti.

(iv) Samaki hao wametoka baharini wanakimbilia sokoni shairi la "Samaki Wamekasirika" (Uk.78, Ub.1, mstari wa 2).

(v) Papa wanalalamika mikuki inawauma "Samaki Wamekasirika" (Uk.78, Ub.3, mstari wa 1).

(vi) Dagaa kachachamaa, lini atasoma shule "Samaki Wamekasirika" (Uk.78, Ub.4, mstari wa 1).

(vii) Mila kushika hatamu "Utamaduni" (Uk.47, Ub.3, mstari wa 3).

(viii) Kiswahili damu, inayonipaka rangi, "Kiswahili" (Uk.50, Ub.1, mstari wa 3).

(ix) Midomo itakucheka shairi la "Chokochoko ya Haki" (Uk.79, Ub.5, mstari wa 3).

**(d) Takriri**

Ni mbinu ya kisanaa ya kurudiarudia kitu au jambo katika kazi ya fasihi kwa lengo la kusisitiza linalosemwa, na zina kazi zifuatazo:-

(a) kupamba kazi ya fasihi;
(b) kusaidia muundo wa shairi;
(c) kusisitiza jambo;
(d) kusaidia kuweka kumbukumbu.

**(e) Takriri neno:**

- Pokea, pokea wito, mambo sasa yako moto shairi la "Ardhi Ujitazame" (Uk. 21, Ub. 3, mstari wa 1).

- Mjukuu, mjukuu, wanjua bambalawe shairi la *"Mawe ya Kale"* (Uk.81, Ub.2, mstari wa 1).

- Haliwi, haliwi ndio nitakalo kuwa kilio shairi la *"ArdhiUujitazame"* (Uk.21, Ub.1, mstari wa 3).

- Utu (shairi la "*Utu ni Nini*" (Uk. 36).
  Utu ni kiumbe hai -------------------------------------------
  Utu kamwe haudai ------------------------------------------
  Utu ni ule uhai, ---------------------------------------------
  Utu wowote wa mtu, -----------------------------------------

- Samaki hao samaki shairi la "*Samaki Wakasirika*" (Uk.78, Ub.1, mstari wa 1).

- Twende twende wajamaa shairi la "Wito Wake Mwenyekiti" (Uk.83, Ub.7, mstari wa 1).

- Viongozi rusha rusha shairi la "Wito Wake Mwenyekiti" (Uk.83, Ub.11, mstari wa 4).

- Hao nyani wanaruka ----------------------------------------
  Hao nyani wanabweka --------------------------------------
  Hao nyani waanguka -----------------------------------------

- Shairi la "Msitu Haukamiliki" (Uk.67, Ub.1, mstari wa 1-3).

- Sione katika shairi la *Usione Ukadhani* (Uk.26).

**(f) Takriri vina**

Hizi ni takriri zilizojitokeza kwa wingi katika diwani hii. Mfano "Njooni Watanzania Kusini" (Uk.39, "ni" ni takriri vina; na kadhalika.

**(g) Takriri kituo:**

"Njooni Watanzania Kusini" (Uk.39)
"Kufundisha Kiswahili" (Uk.54)
"Chokochoko ya Haki" (Uk.79 - 80)

**(h) Takriri vokali**

Mashairi ya "Mawe ya Kale" (Uk.81, Ub.4 "oo" na Ub.2 "uu")

**(i) Tanakali Sauti**

Mwigizo wa sauti ya vitu mfano te—te—te— shairi la "Hutaniacha Morogoro" (Uk.42 ub 11 mstari 1)

**Methali**

- Kweli chema hakidumu.
- Kila avumapo papa ......... "Utenzi wa hayati Sokoine" (Uk.68).

**Nahau**

Katutoka maana yake kafariki - Utenzi wa hayati Sokoine (Uk.68).

**Msemo**

- Fitina ngozi ya tembo (shairi la fitina Uk.14 ub.1)
- Fitina titi la paka halifai kwa mtindi (shairi la *fitina* Ub.1) mstari wa mwisho.
- Wenye nguvu hula sana.

**Lugha za kikabila**

- Lugha za kikabila maneno kama ijatulye, msagule, mulole, kuliyamba, niwagambile, hamuwasile n.k.

Lugha ya kiarabu
Sufufu
Satna

Utohozi wa maneno. Utenzi kuhusu lugha ya Kiswahili (Uk.58, Ub.16).

- Swahili - kutokana na neno suahel lenye asili ya Kiarabu.

- Baraka
  dhihaka — Ub. 24. Yametoakana na Kiarabu

- Shule
  hela — (Ub. 31) Yametokana na Kijerumani

- drili
  shilingi
  skuli
  benki
  skeli — (Ub. 38) Yametokana na Kiingereza.

**Ujenzi wa Taswira**

Katika diwani hii, mashairi mbalimbali yametumia taswira katika kufikisha ujumbe wake. Katika shairi la "Nyoka amegonga Mbuzi' (Uk.77 - 78), msanii ametumia taswira ya nyoka, mbuzi na siafu. "Nyoka" anaashiria uchumi wa nchi na "siafu" anaashiria wananchi. Katika shairi la "Samaki Wakasirika" (Uk.78-79), ametumia "samaki", kuwakilisha raia waliomo katika nchi fulani, Raia hao wako katika rika tofauti. Msanii amewatofautisha kwa kuwaita 'papa' wale 'wazee' wanaorodheshwa na yatendwayo na 'binadamu' ambao ni viongozi au tabaka tawala. Wale wadogo wanawakilishwa na 'dagaa' ambao hao hawajui kinachoendelea, kutaka huduma zitolewe mf. elimu. Picha nyingine ni sokoni, maofisi mbalimbali ya viongozi wanakofanyia kazi na bahari ikiwakilisha nchi ambamo jamii hiyo huishi.

Taswira nyingine ni ya 'chawa'. Katika shairi la "Chawa Aliye Kichwani" (Uk.15), mwandishi ametumia picha ya chawa kuashiria kwamba kimsumbuacho mtu huwa hakitoki mbali. Picha hii ni sawa na methali isemayo kikulachao ki nguoni mwako."

Taswira nyingine zinapatikana katika shairi la "Simba Kukaa na Nyani" (Uk.16). Taswira alizotumia ni simba, mwenye, nyumba na nyani kuashiria wapangaji.

Mloka ni mahiri wa kutumia taswira mbalimbali. Mengi ya mashairi yake yamepambwa kwa taswira mbalimbali. Hizo ni baadhi tu ya taswira zilizotumika katika diwani yake.

Baada ya kuangalia vipengele hivyo, hebu sasa tuone kufanikiwa au kutofanikiwa kifani na kimaudhui kwa mwandishi.

**Kufanikiwa**

Mwandishi amefanikiwa kimaudhui katika kujadili masuala mbalimbali yanayojitokeza katika maisha ya wanajamii hasa katika kipengele cha maadili mema na maonyo, ukombozi kiutamaduni, kiuchumi, kisiasa na uongozi na matatizo mbalimbali yanayokabili nchi yetu.

Aidha, mwandishi amefanikiwa kifani kutokana na jinsi alivyotumia mbinu au stadi katika kufikisha ujumbe kwa walengwa. Mloka amefanikiwa kuonyesha umahiri wake kwa kutumia tamathali za semi, picha na taswira, mafumbo, nahau, misemo, methali, n.k. Amefaulu pia kutumia kanuni za kimapokeo katika kazi yake.

**Kutofanikiwa**

Licha ya kufanikiwa kwa kiasi hicho, mwandishi ameonekana kuwa na dhana potofu kuhusu ushairi. Anadai ushairi ni kipaji kutoka kwa Mungu. Msanii anasema hayo kwenye shairi la "Alimu wa Kiswahili" (Uk.51 – 53, Ub.7).

"Bila shaka twaamini, ushairi ni kipaji kitokacho kwa manani, wachache kuwafariji yatubidi kuthamini, tulivikwa hili taji."

Vilevile msanii ameshindwa kutoa suluhisho yakinifu ili kuondokana na hali ngumu ya maisha kwani njia ya kilimo na kufanya kazi kwa bidii pekee havitoshi, kwani toka zamani watu hulima na kufanya kazi kwa bidii lakini hali zao bado ni duni.

### 12.2.8 ZOEZI LA PILI

*Jibu maswali yafuatayo kisha linganisha majibu yako na yale yaliyotolewa katika kijitabu hiki*

1. Kwa kutumia Diwani ya *Mashairi ya Mloka* taja tofauti iliyopo kati ya mashairi ya mtindo wa kimapokeo na yale ya usasa.

2. Ni vipengele vipi vinavyoangaliwa katika fani unapohakiki muundo wa ushairi.

3. Taja vipengele mbalimbali vya lugha vilivyotumiwa na Mloka katika diwani yake.

## 12.2.9 MUHTASARI WA SEHEMU YA PILI

Fani ni sanaa au ufundi anaoutumia fanani (mtunzi) kufikisha kile anachokusudia kuipelekea jamii inayohusika. Katika ushairi hususani katika kuhakiki kazi za ushairi. Fani hujumuisha muundo, mtindo na matumzi ya lugha.

Matumizi ya lugha hujumuisha misemo, nahau tamathali za semi, kama vile takriri, tashbiha, tashihisi, sitiari, tasfida; n.k. Halikadhalika, matumizi ya lugha hujumuisha lugha ya mkato, lugha ya kigeni, methali, mafunzo au vitendawili, lugha za lahaja, kutohoa na msamiati.

Muundo wa vitabu vya ushairi huzingatia matumizi ya mizani, vina, idadi ya beti na idadi ya mistari. Wakati ambapo mtindo wa ushairi ni wa aina mbili, yaani wa kimapokeo na ule wa kisasa. Mtindo wa kimapokeo huzingatia urari, (mpango) na utaratibu wa mizani, vina, mistari na beti. Yale yaliyofuata utaratibu huo hujulikana kama mashairi ya kisasa.

Kwa ujumla, fani aliyotumia Charles Mloka katika diwani yake imeifanya kazi yake kueleweka vizuri. Kwa kiasi kikubwa, Mloka ametumia mtindo wa kimapokeo, tamathali za semi za kutosha; pia msamiati wa kutosha umetumika na hivyo kutoa mchango mkubwa katika kukikuza na kuiendeleza lugha ya Kiswahili.

### 12.2.10 MASWALI YA KUTUMA KWA MKUFUNZI

*Jibu maswali yafuatayo kwenye kitabu cha mazoezi ulichopewa kisha kitume kwa Mkufunzi kwa masahihisho*

1. Fafanua jinsi utumiaji wa taswira katika "*Diwani ya Mloka*" ulivyofanikiwa kufikisha ujumbe kwa jamii.

   **[Alama 20]**

2. Mwandishi wa "*Diwani ya Mloka*" amefanikiwa kuelimisha jamii katika masuala ya siasa, mapenzi utamaduni na uchumi. Jadili usemi huu ukizingatia diwani hii.

   **[Alama 20]**

3. Ushauri bora ni ule unaotumia picha na tamathali za semi. Jadili jinsi kauli hii inavyoathibitishwa katika "*Diwani ya Mloka.*"

   **[Alama 20]**

4. Mashairi ya "*Diwani ya Mloka*" hayana umuhimu wowote katika Tanzania ya leo Jadili.

   **[Alama 20]**

5. Jadili ujumbe uliojitokeza katika mashairi ya "*Diwani ya Mloka.*"

   **[Alama 20]**

### 12.2.11 MUHTASARI WA SOMO LOTE

Ndugu Mwanafunzi, umekwisha jifunza, katika uchambuzi wa ushairi wa fasihi andishi umejifunza kwamba ni vipengele viwili tu vinavyotuongoza katika uhakiki wa kazi hizi za fasihi andishi. Navyo ni maudhui na fani. Upande wa maudhui tunaangalia na kuchambua masuala (maudhui) mbalimbali yanayojadiliwa na mtunzi. Mhakiki hujafungwa kujadili na kuhakiki maandishi ya mtunzi, kosoa pale unapoona mtunzi ametoka nje ya maadili ya jamii inayohusika. Pia, angalia je, yanayozungumzwa yana uhusiano gani na maisha halisi ya jamii? Kwa kufanya hivyo utakuwa na upeo mpana wa uchambuzi.

Kwa upande wa fani inakupasa kuzingatia kwamba hata kama mtunzi amejitahidi sana kuandika maudhui yake lakini kumbuka kwamba fani na maudhui ni pande mbili za sarafu. Kamwe huwezi kuvitenganisha vitu hivyo viwili. Kwa hiyo, lazima uvichambue ipasavyo ni kwa namna gani mtunzi ametumia lugha kufikisha maudhui kwa jamii anayoiandikia. Pia, mtindo, muundo gani umetumika? Hapo utakuwa umeiangalia fani katika ushairi wa fasihi andishi.

Hali kadhalika, wakati na kabla ya kuanza kuchambua kitabu chochote cha fasihi andishi, inakupasa uzingatie jina la kitabu, picha iliyopo kitabuni; pamoja na utangulizi wa kitabu. Tujiulize, je, vinatoa taswira gani au picha gani ya yaliyomo.

## 12.2.12 MAJIBU YA MAZOEZI

**Zoezi la Kwanza**

1. Dhamira
    - utamaduni
    - umuhimu wa kufanya kazi
    - umuhimu wa elimu
    - nafasi ya mwanamke
    - mapenzi
    - maombolezo
    - maadili mema na maonyo
    - kuinua uchumi; n.k.

2. Diwani ni mkusanyiko wa mashairi, tenzi, mashairi na tenzi zilizotungwa na mwandishi mmoja tu kwa nyakati tofauti na mwishowe kukusanywa na kuwekwa pamoja na kuunda kitabu.

3. Maadili/ujumbe
    - Ubinafsi, fitina, sifa mbaya na kashfa ni chanzo cha chuki, choyo, wivu na tamaa mbaya katika jamii.
    - Elimu ni ufunguo wa maisha.
    - Ili kuinua uchumi wetu hatuna budi kufanya kazi.
    - Tudumishe utamaduni wetu ikiwemo lugha ya kiswahili.
    - Elimu tu haitoshi lazima kuwepo na hekima. Hivyo hekima ni zaidi kuliko elimu.

4. Kundi (i) Maisha ya maadili na mawaidha
   (ii) Mashairi ya lugha na fasihi.
   (iii) Mashairi ya siasa na uchumi.

**Zoezi la Pili**

1. Mtindo wa kimapokeo hufuata urari wa vina na mizani
    - matumizi ya mizani 16 kwa kila mshororo
    - matumizi ya vina vya kati na vya mwisho
    - idadi ya mistari, idadi ya mistari ni ile inayokidhi kanuni za mashairi ya kimapokeo. Mistari 2 – 6.
    - Mtindo wa usasa haufuati utaratibu wa vina na mizani, pamoja na mistari.

2. Vipengele vianvyohakikiwa katika muundo wa ushairi ni:
   - matumizi ya mizani
   - idadi ya mistari
   - matumizi ya vina
   - mpangilio wa beti.

3. Vipengele vya matumizi ya lugha vilivyotumika ni msamiati, methali, nahau, misemo, tamathali za semi, lugha ya mkato, picha na taswira, utohozi, lugha ya lahaja mbalimbali, nk. Mifano yake ni kama ilivyoainishwa kwenye somo.

### 12.2.13 FARAHASA

**Danguro** - Nyumba wanayokaa malaya.

**Mkururo** - Mfuatano wa vitu au watu (Uk.16, Ub.1, mstari 8)

**Jopo** - Kundi la watu waliokusanyika pamoja (Uk.89, Ub.12, mstari wa 2).

**Dhihaka** - Maneno au vitendo vya kufanya mzaha au utani (Uk.85, Ub.11, mstari wa 2).

**Johari** - Kitu cha thamani (Uk.50, Ub.4, mstari wa 5).

### 12.2.14 MAREJEO

Mloka, C. *Diwani ya Mloka,* 1988 Benedictive Publications

Ndanda Peramiho, Tanzania.

## SOMO: 12.3

## UHAKIKI WA MASHAIRI YA MALENGA WAPYA

## YALIYOMO

**UKURASA**


12.3 Uhakiki wa Kitabu cha Mashairi ya Malenga Wapya ... 60
12.3.1 Utangulizi wa Somo ... ... ... ... ... ... 60
12.3.2 Malengo ya Somo ... ... ... ... ... ... 60
12.3.3 Utangulizi wa Kitabu ... ... ... ... ... ... 61
12.3.4 Sehemu ya Kwanza: Maudhui ... ... ... ... ... 61
12.3.5 Zoezi la Kwanza ... ... ... ... ... ... ... 72
12.3.6 Muhtasari wa Sehemu ya Kwanza ... ... ... ... 73
12.3.7 Sehemu ya Pili: Fani ... ... ... ... ... ... 74
12.3.8 Zoezi la Pili ... ... ... ... ... ... ... 83
12.3.9 Muhtasari wa Sehemu ya Pili ... ... ... ... ... 84
12.3.10 Zoezi la Kutuma kwa Mkufunzi ... ... ... ... 85
12.3.11 Muhtasari wa Somo Lote ...... ... ... ... ... 86
12.3.12 Majibu ya Mazoezi ... ... ... ... ... ... ... 87
12.3.13 Marejeo ... ... ... ... ... ... ... ... 89

## 12.3 UHAKIKI WA KITABU CHA MASHAIRI YA MALENGA WAPYA

### 12.3.1 UTANGULIZI WA SOMO

Mpendwa mwanafunzi, umemaliza Somo la Pili katika mfululizo wa masomo ya kuchambua vitabu teule vya ushairi. Ni matumaini yangu kuwa umenufaika sana na somo hilo na umelielewa vyema. Sasa tunaanza Somo la Tatu na la mwisho katika mfululizo huu.

Katika somo hili utajifunza uhakiki wa ushairi katika kitabu cha *Malenga Wapya*. Kama kawaida, somo hili limegawanyika katika sehemu kuu mbili, yaani Sehemu ya Kwanza itahusu uchambuzi wa vipengele vya maudhui na Sehemu ya Pili itahusu uchambuzi wa vipengele vya fani, bila kusahau mazoezi ya kujipima. Aidha, kutakuwepo na mazoezi ya kutuma kwa mkufunzi na yale ya kujiandaa kwa mtihani wako wa mwisho. Mwisho, tutatoa tathmni kuhusu mwandishi alivyomudu au kutomudu vipengele vya fani na maudhui.

### 12.3.2 MALENGO

Baada ya kusoma na kumaliza somo hili utaweza:

- kutaja na kufafanua kwa mifano dhamira mbalimbali zilizomo katika *Malenga Wapya;*
- kutaja na kufafanua vipengele mbalimbali vya fani kama vilivyotumiwa na wandishi wa *Malenga Wapya;*
- kutathmini kufaulu au kushindwa kwa waandishi katika kuvimudu vipengele vya fani na maudhui; na
- kujibu maswali yoyote na, hasa, ya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne katika ushairi wa Kiswahili.

### 12.3.3 UTANGULIZI WA KITABU

Mpendwa mwanafunzi, katika sehemu hii tutajadili maudhui ya kitabu cha *Malenga Wapya*. Ni vizuri tukijikumbusha maana ya maudhui kuwa ni jumla ya mambo yanayoelezwa na mtunzi au yanayojitokeza katika kazi ya fahisi. Aidha, dhana hii hujumuisha dhamira, ujumbe na maadili.

### 12.3.4 SEHEMU YA KWANZA: UCHAMBUZI WA MAUDHUI

Katika kuichambua kazi hii tutaanza na dhamira. Dhamira katika kazi ya fasihi ni wazo kuu au jambo lililomsukuma mtunzi hadi kufikia kuitunga kazi yake. Mara nyingi kazi yoyote ya fasihi huwa na dhamira kuu na dhamira ndogondogo. Katika *Malenga Wapya* dhamira zilizojitokeza ni nyingi. Hivyo, haitakuwa rahisi kwetu kueleza kila kitu. Aidha, wewe kama mwanafunzi katika fasihi jitahidi kuchambua kitabu hiki ili kupanua mawazo yako na kujiongezea yale utakayobaini kuwa hayajaongelewa.

**Dhamira**

Miongoni mwa dhamira zilizojitokeza ni pamoja na kuinua uchumi, kilimo, uongozi mbaya, maadili, kutenda haki, ukombozi, usaliti, nafasi ya mwanamke, mapenzi na ndoa, matabaka, matumizi ya fedha, umuhimu wa kutatua matatizo na athari za sukari mwilini.

Sasa hebu tuchambue dhamira moja baada ya nyingine.

**Umuhimu wa Kuinua Uchumi**

Mtunzi wa *Malenga Wapya* anaonyesha kuwa kujenga uchumi imara ni kujenga taifa lenye uwezo na la kujitegemea. Katika shairi la "Adui" (Uk.131) wasanii wanaonyesha umuhimu wa kuinua kilimo ili kuondokana na adui njaa:

*"Tulime jama tulime, tushinde adui njaa,*
*Hapa kwetu ituhame, kwingine kutokomea,*
*Wala sisi tusikome, chakula kujilimia,*
*Tutie jembe mpini, tuteremke shambani." (Ub.4)*

*"Chakula kujilimia, ziada kujipatia,*
*Tuache kutegemea, vya nje kuagizia,*
*Siku watojigomea, nani tutamlilia,*
*Tutie jembe mpini, tuteremke shambani." (Ub.5)*

Katika beti hizi mbili umuhimu wa kilimo katika kujenga uchumi imara na taifa litakalojitegemea kwa chakula unasisitizwa.

Aidha, shairi la "Mkulima" (Uk.3) linamwonyesha mkulima kama mtu duni likimlinganisha na watu wengine. Huyu ni mtu ambaye analima ili kulisha watu wote nchini na kuinua pato la taifa lakini hathaminiwi na watu wanaohusika. Tunaambiwa:

*"Wakazi wa mjini, na wafanyakazi pia,*
*Na viongozi nchini, hudumu awapatia,*
*Sijui kakosa nini, thamani kutomtia,*
*Mkulima naye mtu, yafaa kuthaminiwa." (Ub.5)*

Hivyo, ili kuimarisha uchumi wetu ni lazima tumthamini mkulima na kumpatia huduma muhimu anazostahili, kwani chakula kipunguapo nchini anayetupiwa lawama ni mkulima, kama wasemavyo washairi:

*"Upungufu wa chakula, utokeapo nchini,*
*Hukumbana na suala, shambani wafanyanini,*
*Kazi yako unalala, watia njaa nchini*
*Mkulima naye mtu, yafaa athaminiwe." (Ub.7)*

Pamoja na juhudi zake katika kuinua uchumi na nchi, mkulima hapewi huduma muhimu badala yake huduma hizo hupatikana kwa wale waishio mijini. Waandishi wanasema:

*"Starehe kwa jumla, zinaishia mjini,*
*maji safi ya muala, njia na umeme ndani,*
*aliyezichuma hela, ni mkulima shambani,*
*mkulima naye mtu, yafaa athaminiwe." (Ub.8)*

Hapa tunaoneshwa kuwa matunda ya kazi ya mkulima huwanufaisha zaidi watu wa mjini.

Katika suala la kuinua uchumi, waandishi pia wanasisitiza umuhimu wa kufanyakazi kwa pamoja raia na viongozi, katika shairi la *"Tuyazingatie haya"* (Uk.27).

*"Uchumi kufufua, si hotuba refu sana,*
*moja litosaidia, ni kwa kuhamasishana,*
*jingine linalofuatia, sote kushirikiana,*
*tuyazingatie haya, wala tusirudi nyuma." (Ub.2)*

**Nafasi ya Mwanamke katika jamii**

Mwandishi anasisitiza kuwa mwanamke akikombolewa jamii nzima itakuwa huru. Sasa mwanamke amechoka kufungiwa ndani, anaona ni wakati anaopaswa kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa ili kuleta maendeleo. Mawazo haya tunayapata katika shairi la "Kifungo." Mwandishi anasema:

*"Kwa kuwa ni mwanamke, ndani mwanifutika,*
*lazima nje nitoke, kupata ninayotaka,*
*nimechoshwa na upweke, sitaki kudhalilika,*
*kifungo kimenichosha, minyororo nafungua." (Ub.7).*

Nalo shairi la "Hina Inapapatuka" (Uk.58) linatuonyesha hadhi aliyopewa mwanamke hapo zamani. Linasema;

*"Zamani tukikumbuka, watiaji walivia,*
*nyumbani katu kutoka, ndani walijichimbia*
*mabwana walitamka, marufuku kutembea,*
*unyonge inaondoa, hina inapapatuka." (Ub.2)*

Hapa mwandishi anatuonyesha jinsi ambavyo mwanamke hakuruhusiwa kutoka nje kwa matembezi. Kazi yake kubwa ilikuwa ni kupika chakula, hakuruhusiwa kabisa kusoma na kuandika.

Kwa upande mwingine, mshairi anatuonyesha jinsi mabadiliko ya kiuchumi, siasa na kiutamaduni yanavyomkomboa mwanamke hatua kwa hatua. Kwa wakati huu, wanawake wanashiriki katika kazi mbalimbali zilizosadikika kuwa kazi za wanaume wakati huo. Katika beti hizi mbili tunaelezwa:

*"Leo wanamakanika, hadhi yao kutetea,*
*kila mahali kufika, na wao wameenea,*
*kazini wajumuika, shime wanajifanyia,*
*unyonge inaondoa, hina inapapatuka." (Ub.7)*

*"Kila utapopashika, nao wameshafika,*
*zege inapopondeka, ni wao hujipondea,*
*matofali kupeleka, mafundi kusaidia,*
*unyonge inaondoa, hina inapapatuka." (Ub.8)*

Pia katika shairi hili waandishi wanatoa rai kwa wanawake kuendelea kushikilia msimamo walio nao (kukaza uzi) ili wafikie ukombozi wa kweli. Haya tunayapata katika ubeti ufuatao:

*"Nasaha ninatamka, mabibi ninawambia,*
*uzi mulioushika, msije kuuwachia,*
*ogopeni kina kaka, yenu kutowavunjia,*
*unyonge inaondoa, hina inapapatuka."* (Ub.14)

**Ukombozi**

Hii ni dhamira nyingine inayojitokeza katika *Malenga Wapya.* Katika kuielezea dhamira hii watunzi wamegusia masuala mbalimbali yaihusuyo jamii, kiuchumi kisiasa, kiutamaduni, na kifikira. Katika shairi la "Tunzo" (Uk.29) kwa mfano, tunaonyeshwa historia ya tulikotoka, hapa tulipo na tunakoelekea. Katika ubeti wa tatu tunasoma:

*"Ni la uchumi anguko, hivi sasa tumekwama, kuongoza,*
*Maradhi kwetu yawako, hata yale yasopona ni jalizo*
*Ujinga bado uwako, kuna wale wasosoma, kigezo."*(Ub.3)

Hapa tunaonyeshwa kuwa jamii inapaswa kujikomboa kiuchumi, kiafya na kielimu ili kuondokana na adui ujinga. Mwandishi anashauri jamii nzima ishirikiane ili kuondokana na matatizo yaliyopo. Aidha, anahimiza jinsi ya kujikwamua kwa kuweka sera, malengo na mwelekeo wenye kuishirikisha jamii nzima. Anasema:

*"Kwenu ninalo tamko, kwa sote jamii nzima, fuatizo,*
*sote tuwe unganiko, kina baba kinamama, ni himizo,*
*tuondoshe sawijiko, ili yapate tuhama, matatizo."* (Ub.6)

Katika kuongelea ukombozi wa kiuchumi mwandishi ametumia shairi la "Sokomoko Baharini." (Uk.63) Shairi hili linazungumzia kitaswira ukombozi wa kiuchumi hapa nchini.

Aidha, shairi la "Samaki Mtungoni" (Uk.19) linaonyesha harakati za watu wa tabaka la chini kuondokana na utumwa wa kutawaliwa na mkoloni au tabaka tawala. *Samaki* anaashiria watu wa tabaka tawaliwa (la chini) wanaonyonywa na kugandamizwa; na mvuvi ni tabaka tawala (la juu). Wasanii wanatoa hadhari kwamba licha ya kupata uhuru wananchi wanataka kujihami dhidi ya ukoloni mamboleo. Ukombozi huu ni wa kisiasa na kiuchumi.

Ukombozi pia umeonyeshwa katika ngazi ya mtu binafsi. Msanii anaonesha umuhimu wa ukombozi wa kifikra katika shairi lake la "Usiwe Bendera." (Uk.31) Jamii inatahadharishwa isiwe

bendera kufuata kila uwelekeo wa upepo; bali ijitegemee kimawazo. Anasema:

*"Tuma fikirazo, pima yanofaa,*
*tazama kikwazo, wapi chatokea,*
*pima na uwezo, wa kukifanyia,*
*usiwe bendera, kufata upepo." (Ub.3)*

Katika maudhui ya *Malenga Wapya*, limo pia suala la matabaka. Wasanii wanaonyesha maisha waishio watu wa tabaka la chini na mahusiano yao na wale wanaowatumikisha yaani tabaka la juu. Mawazo haya yapo katika shairi la "***Punda***" (Uk.23) wanaposema;

*"Toka ulipozaliwa, maishayo ni kizogo,*
*hujapata kuenziwa, waishi tirigivyogo,*
*nawe hujajielewa, u kiumbe hu kigogo,*
*kama ungefadhiliwa, usingebeba mizigo,*
*hakika ulionewa, hustahili kipigo,*
*haki umeitambua, idadi japo kidogo."*

Hapa tunaonyeshwa jinsi tabaka la chini linavyotumikishwa kwa kulinganishwa na punda.

Pia suala la matabaka linadhihirika katika shairi la "Nini wanangu" (Uk.26) wasanii wanasema:

*"Niseme nini wanangu, wasikie wahusika,*
*Nikitoa neno langu, kathiri hughadhibika,*
*Koo mefanya furungu, kwa kushindwa kutamka*
*Sitegemei nafuu! (Ub.3)*

Katika shairi hili tunaonyeshwa hali ilivyo ngumu na duni kwa tabaka la chini. Aidha, linafafanua jinsi wasivyokuwa na nafasi ya kutoa mawazo waliyonayo.

**Uongozi mbaya**
Hii ni dhamira nyingine inayojadiliwa katika kitabu hiki. Waandishi wanaonyesha jinsi viongozi walio madarakani wasivyojali maslahi ya watu wengine, kiasi kwamba badala ya kusonga mbele tunazidi kudidimia kimaendeleo. Haya tunayapata katika shairi la "Hali halisi" (Uk.5):

*"Hali hii yashangaza, nasi imetulemaza,*
*imekuwa miujiza, yafaa kujiuliza,*
*mshumaa unawaka, giza mbona linazidi? (Ub.1)*

Vilevile, katika shairi la "Puuzo" (Uk.8) waandishi wanatuonyesha jinsi wale wenye nafasi au madaraka ya kuitumikia jamii, wasivyotekekeleza wajibu wao kikamilifu. Viongozi katika shairi hili wanaonyeshwa kuwa watu wasiojali wenzao hasa wale wanaokuwa na shida waendapo kuwaona ofisini kwao. Washairi wanasema:

*"Unapokuwa na shida, wao wanakupuuza,*
*wanajitia kidada, na kuifanya ajiza,*
*wajifanya hawajali."* *(Ub.2)*

*Ofisini ukifika, wanakuweka baoni,*
*Wakati uliofika, wao hawauthamini,*
*Wanakwambia subiri."* *(Ub.3)*

Mashairi mengine yanayohusu suala la uongozi mbaya ni pamoja na "Bahari" (Uk.6). Hili linaonesha dhuluma ya viongozi kwa wananchi, waandishi wanasema:

*"Hudai ni haki yao, mola amewajalia,*
*Kuwadhulumu wenzano, wao wanafurahia,*
*Nao kwa unyonge wao, wadogo wateketea,*
*Bahari ina hatari, wala usiichezee."* *(Ub.7)*

Nalo shairi la "Mpaka lini" (Uk.49) linaonyesha jinsi viongozi wasivyosikiliza matatizo ya raia ili kuyatatua. Linaeleza pia jinsi viongozi wanavyowakumbatia wasema uongo huku wakiwanyanyasa wasema ukweli. Wanasema:

*"Msema kweli, kwenu nyinyi ni chagizo,*
*mtaka hali, havuki mbele ya vikwazo,*
*mwongo sana, kwenu nyinyi ni kigezo,*
*mpaka lini mtatuchezea?"* *(Ub.2)*

*Mpaka lini, dhiki hii itafishwa,*
*Hadi lini mnyonge atadunishwa,*
*jambo hili halinabudi kukomeshwa,*
*Mpaka lini tutasemewa?"* *(Ub.3)*

Kadhalika, katika shairi la "Payuka" (Uk.50) mwandishi anaonyesha jinsi viongozi wanavyopayuka ovyo. Huku wakiahidi mambo mengi wakiwa majukwaani pasipo kuyatekeleza. Badala yake hubaki kuwanyonya na kuwanyanyasa wananchi. Katika ubeti wa pili mwandishi anasema:

*"Kupayuka kwenu huko,*
*mbona tu kokoriko,*
*sioni linalokuwa."*

**Umuhimu wa Kutenda Mema (maadili mema)**
Waandishi wanatoa maadili mbalimbali yanayowahimiza wanajamii kuwa waadilifu, wanaamini kuwa ni muhimu sana kutenda matendo mema na kuepuka maovu ili kuifanya jamii iishi kwa amani na utulivu.

Mashairi yenye kuadilisha ni pamoja na "Ulimi" (Uk.41) Katika shairi hili wanajamii wanashauriwa kuzichunga ndimi zao ili zisiseme mambo mabaya yenye kuifarakanisha jamii. Washairi wanasema:

*"Usiropokeropoke, kwa wenzio kwanza sema,*
*Usipachikepachike, maneno yasiyo mema,*
*Useme wanufaike, kwa kauli yako njema,*
*Ewe ulimi sikia! (Ub.3)*

Katika shairi la "Siharakie maisha" (Uk.11), waandishi wanawaasa wanajamii na hasa vijana walio masomoni kutokuwa na pupa ya maisha na kutamani mambo makubwa yasiyowiana na umri wao. Washairi wanasema;

*"Ubado ni mwanafunzi, usiingiwe na simanzi,*
*ruka vikwazo ja panzi, uipambe yako enzi,*
*maisha safari ndefu, kutembea usichoke," (Ub.2)*

Vilevile, lipo shairi la "Maisha ni Kama Njia"(Uk.40) ambalo linasisitizia jamii kuhusu umuhimu wa kutenda mema na kuepukana na maovu. Washairi wanaona kuwa ubabe na kiburi ni vitu visivyosaidia lolote maishani wanasema:

*"Iweze yako suduri, binadamu zingatia,*
*kaa ukitafakari, utende yalo sawia,*
*ubabe au kiburi, havitokusaidia,*
*maisha ni kama njia, tukumbuke akhiria." (Ub.3)*

Wanaendelea kusema;

*"Wenzako usiwabari, kuwatendea kadhia,*
*kwako lofa na tajiri, vyema kuwafikiria,*
*yupi atakusitiri, humjui abadia,*
*maisha ni kama njia, tukumbuke akhiria." (Ub.4)*

Shairi jingine linaloongelea suala la maadili ni "Hisani Hulipwa." Katika shairi hili washairi wanabainisha kuwa katika maisha rafiki wa kweli ni yule anayekusaidia wakati wote wa shida na raha. Tunasoma:

*"Akuulizae, uwapo na shida,*
*Akuteteae, ukishambuliwa,*
*Akumulikae, uwapo gizani,*
*hisani hulipwa." (Ub.1)*

*Akukopeshae, hutaka kulipwa,*
*Akuazimae, ujue rejesha,*
*Akugaiae, anae safi roho,*
*lakini hisani hulipwa." (Ub.4)*

**Mapenzi na Ndoa**
Dhamira hii imejitokeza katika *Malenga Wapya* katika sura mbalimbali. Kwanza, washairi wameonyesha mapenzi ya kujali pesa. Wanaeleza kuwa mapenzi ya siku hizi hayana thamani katika jamii kutokana na kwamba pesa imewekwa mbele na hivyo mapenzi kuwa bidhaa ya kununuliwa. Pili, washairi wanaonyesha jinsi ndoa ilivyo muhimu katika jamii.

Mashairi yanayoongelea suala la mapenzi na ndoa ni pamoja na *"Ua"* (Uk.21). Katika shairi hili ua limewakilisha mtu, yaani msichana ambaye kadri anavyokuwa ndivyo anavyopendeza na kuwavutia wanaume. Kwa lugha ya picha msanii anatueleza jinsi tunavyowajibika kuwatunza wenzi wetu tangu mwanzo wa mahusiano hadi tunapoamua kuishi pamoja. Anasema:

*"Ua nililimiliki, toka halijachanua,*
*Sasa lina washabiki, wote wanalirandia,*
*Ua sasa limepea, macho walikodolea." (Ub.2)*

*"Nami sitoliachia, matunzo talipatia,*
*Hadi nitapofikia, mkononi kulitia,*
*Ua sasa limepea, macho walikodolea." (Ub.7)*

Pia katika shairi hili msanii anatuonyesha kuwa pindi mtu anapofikia umri wa kuoa au kuolewa ni sharti afanye hivyo.

Akiongelea dhana ya mapenzi ya ulaghai au ya kujali pesa, msanii anatumia shairi la "Utanikumbuka" (Uk.44); anasema:

*"Yeye amekuhadaa, nawe tele ukajaa,*
*Ukajitia tamaa, na kujawa na fazaa,*
*Ulafi umekuvaa, vyake unang'ang'ania*
*Limbukeni umekuwa, vitu unaajabia." (Ub.2)*

Katika ubeti huu tunaonyeshwa kuwa mtu amempenda mwenzake kwa tamaa yake ya mali.

Vilevile, washairi wanakemea tabia mbaya ya baadhi ya wanaume wasiojali wake zao na kupoteza muda mwingi na wanawake wengine. Katika shairi la "Kwanini" (Uk.1), tunasoma:

*"Japo yeye, ana wake, sheriani.*
*Ni ladhaye, amshike, wa fulani.*
*Shukuruye, ni mateke, kwa wandani*
*Kwanini?" (Ub.3)*

Katika kufafanua jinsi wanaume wa aina hiyo wazitesavyo familia zao washairi wanasema:

*"Mume pesa, apeleke, Chumbageni.*
*Azitesa, toto zake, firauni.*
*Apepesa, mwendo wake, ulevini*
*Kwanini? (Ub.6).*

Mashairi mengine yanayojadili dhamira hii ni "Kuunge" (Uk.25), "Kitendawili" (Uk.14) na "Nipate wapi mwingine?" (Uk.32).

**Umuhimu wa Kutumia Mali Vizuri:**
Dhamira nyingine inayojadiliwa katika *Malenga Wapya* ni muhimu wa kutumia mali vizuri. Waandishi wanakemea tabia ya ufujaji wa mali na kudai kuwa ni kujitafutia umaskini usio wa lazima. Wanatoa maonyo yao kupitia shairi la "Israfu" (Uk.17) wakisema:

*"Mali ulojichumia, ni yako nakubalia,*
*Lakini kiangalia, vipi unaitumia,*
*Mwenzangu nakuusia, Israfu haifai."* (Ub.1)

Wakiendelea kuonyesha madhara ya ufujaji wa mali wanatuambia kuwa ukisha kuwa maskini huwa unakimbiwa na watu hata marafiki zako. Katika ubeti wa nne washairi wanasema:

*"Israfu ikimea, Mali inayoyomea,*
*Watu watakuzomea,Ukikosa egemea,*
*Mwenzangu nakuusia Israfu haifai."* (Ub.4)

**Haki**
Dhamira nyingine ni haki. Katika kitabu hiki washairi wanaonyesha jinsi wanayonge wanavyohaha kuitafuta haki yao huku wakiwashangaa viongozi wao wanavyowasaliti. Haya

tunayashuhudia katika ubeti wa nne katika Shairi la "Haki" (Uk.47) wanaposema:

*"Sio hao mabwana, waloteuliwa, kupata mwangaza,*
*Haki wakubana, lilotarajiwa, kwenye nchi kiza*
*Ndevu kuchomana, wengine kuliwa, tukijiingiza,*
*kambi yatuviza. (Ub.4)*

**Umuhimu wa Kutatua Matatizo**

Zaidi ya hayo, waandishi wa *Malenga Wapya* wameongelea suala la umuhimu wa kutatua matatizo katika jamii. Wameonyesha kuwa tangu kupata uhuru jamii yetu imekuwa ikikabiliwa na matatizo mbalimbali ambayo yamekuwa kikwazo kwa maendeleo ya taifa hili. Wanaonyesha kuwa ongezeko la watu, kuanguka kwa uchumi, maradhi na ubadhilifu ni matatizo yanayohitaji kuondolewa ili tuweze kuendelea. Katika shairi la "Tunzo" (Uk.29) ubeti wa sita wanasema:

*"Kwenu ninalo tamko, kwa yote jamii nzima, fuatizo*
*Sote tuwe unganiko, kina baba kina mama, ni himizo*
*Tuondoshe sawijiko, ili yapate tuhama, Matatizo."*

Hapa waandishi wanatoa wito wa kila mtu kushiriki katika kuondoa matatizo yaliyopo katika jamii.

**Athari za Sukari Mwilini**

Athari za sukari mwilini, hii ni dhamira nyingine iliyojadiliwa na waandishi wa kitabu hiki. Wanakumbusha kuwa japo sukari ni kitu muhimu mwilini, ikizidi huleta madhara makubwa. Wanatoa mifano ya madhara hayo kuwa ni pamoja na kuoza meno, kupata ugonjwa wa safura, katika shairi la "Sukari" (Uk.56) wanasema:

*"Hukupatisha hasara, kila mara kitumia,*
*hukutia na safura, kila leo kijitia*
*tumbo linaweza fura, halafu ukajutia,*
*japo ni tamu balaa, sukari uiogope." (Ub.4)*

Mpendwa mwanafunzi, hizo dhamira zilizojadiliwa ni baadhi tu ya dhamira zinazoweza kubainishwa katika kitabu cha *Malenga Wapya.* Hivyo, upo uwezekano wa kuongeza dhamira nyingine mara unaposoma na kuhakiki kitabu hiki. Kwa hiyo, isichukuliwe kuwa hizo ndizo dhamira pekee zinazojitokeza katika kazi hii.

**UJUMBE/MAFUNZO**

Mpendwa mwanafunzi, baada ya kujifunza mambo yanayozungumziwa katika *Malenga Wapya* (maudhui) kwa upande wa dhamira, sasa tuchambue mafunzo tuyapatayo katika kitabu hiki.

Kwanza, kuinua uchumi wa nchi ni jambo muhimu sana ili kuweza kuondokana na utegemezi wa misaada toka nje.

Pili, kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wetu; hivyo lazima tukiimarishe na kumthamini mkulima.

Tatu, ukombozi wa mwanamke ni suala muhimu sana kwani akikombolewa atazijua na kuzidai haki zake kwa ujasiri na atakuwa msaada mkubwa kwa jamii.

Nne, ni muhimu kutatua matatizo mbalimbali yanayoikabili jamii yetu ili tuweze kuishi kwa amani na utulivu.

Tano, ni vizuri kuwa na maadili mema katika jamii kwani kufanya hivyo kutasaidia kujenga jamii yenye haki na usawa.

Sita, ili kujiletea maendeleo ya kudumu tuepukane na ufujaji au utumiaji ovyo wa mali.

Mwisho, viongozi wawe watendaji kwa vitendo na siyo wapiga porojo tu za majukwaani.

### 12.3.4 ZOEZI LA KWANZA

*Jibu maswali yafuatayo kisha linganisha majibu yako na yale yaliyotolewa katika kijitabu hiki:*

1. Dhamira zilizojitokeza katika Malenga Wapya ni:................ (Taja dhamira tano tu).
   (a) ------------------------------------------------------------
   (b) ------------------------------------------------------------
   (c) ------------------------------------------------------------
   (d) ------------------------------------------------------------
   (e) ------------------------------------------------------------

2. Ni mafundisho gani tuyapatayo kwa kusoma kitabu cha Malenga Wapya? (Taja matano tu).
   (a) ------------------------------------------------------------
   (b) ------------------------------------------------------------
   (c) ------------------------------------------------------------
   (d) ------------------------------------------------------------
   (e) ------------------------------------------------------------

3. Katika shairi hili "***TUNZO***", ubeti wa tatu unaeleza nini?

   *"Ni la uchumi anguko, hivi sasa tumekwama kuongozo,*
   *maradhi kwetu yawako, hata yale yasopona, ni jalizo.*
   *ujinga bado uwapo, kuna wale wasosoma, ndo kigezo".*

### 12.3.6 MUHTASARI WA SEHEMU YA KWANZA

Katika sehemu hii tumejifunza masuala mbalimbali yaliyojadiliwa na washairi waliotunga Malenga Wapya. Masuala hayo (dhamira) ni pamoja na kuinua uchumi, uongozi mbaya, nafasi ya mwanamke, maadili mema, ukombozi, mapenzi na ndoa, haki, matumizi ya mali (pesa), umuhimu wa kutatua matatizo na athari za sukari mwilini.

Hizo ni baadhi tu ya dhamira chomozi katika kitabu hiki. Uzisomapo usisite kuzihusisha na kitabu chenyewe pamoja na ulimwengu halisi tuuishio ili kupata uhalisia wa yale yaliyobainishwa. Ni wazi kuwa ukifanya hivyo utaweza kupanua welevu wako na kuongeza dhamira nyingine zaidi.

Aidha, tumejifunza mafundisho na ujumbe mbalimbali unaoendana na dhamira hizo. Ni imani yetu kuwa utanufaika kwa yote tuliyoyajadili katika tahakiki hii.

## 12.2.7 SEHEMU YA PILI: FANI

### UTANGULIZI

Ndugu mwanafunzi, kwa sasa umemaliza sehemu ya kwanza ya maudhui. Bila shaka, sehemu hiyo imekupa fursa ya kujifunza mambo mbalimbali yaliyojadiliwa na mwandishi katika kitabu.

Karibu tena katika sehemu ya pili ambayo inahusu fani. Katika kipengele hiki tunaangalia ufundi wa kisanii aliotumia mwandishi katika kuisana kazi yake. Katika sehemu hii tunaangalia vipengele mbalimbali vinavyokamilisha fani. Vipengele hivyo ni pamoja na muundo, mtindo, matumizi ya lugha na mandhari. Tuangalie kipengele kimoja baada ya kingine.

**Muundo:** Ni namna kazi ya fasihi ilivyopangwa au ilivyojengwa. Katika kipengele hiki tutaangalia beti, mistari, mizani, vina na kituo. Tuanze kwa kuchambua kimoja baada ya kingine.

**Beti:** Shairi lenye beti chache kabisa katika kitabu hiki ni la ubeti mmoja, mfano shairi la 14 la ***PUNDA*** *(Uk.23)*, na shairi la 29 ***Pasua Uwape Ukweli*** *(Uk.46)*.

**Punda**

*Toka ulipozaliwa,maishayo ni kizogo,*
*Hujapata kuenziwa, waishi tirigivyogo,*
*Nawe hujajielewa, ukiumbe ukigogo,*
*Kama ungefadhiliwa, usingebeba mizigo,*
*Hakika ulionewa, hustahili pigo,*
*Haki umeitambua, idadi japo kidogo.*

Shairi linalofuata kwa kuwa na beti chache ni la 9 "Kitendawili" (Uk.14) lenye beti mbili.

Shairi lenye beti nyingi kabisa ni lile la 32 la "Payuka" (Uk.50) lenye beti 17. Aidha linafuatiwa na shairi "Hina Inapapatuka" (Uk.58) lenye beti 15.

Mashairi mengine katika kitabu hiki yana beti 3, 4, 5, 7, 8, 9, 10, 11 na kadhalika.

**MISTARI:** Mashairi mengi katika *Malenga Wapya* ni yale ya tarbia, yaani yenye mishororo (mistari) minne. Mifano ni kama:

"Majonzi" (6), "Kwa Nini" (1), "Mkulima" (2), "Bahari" (4), "Adui" (8) na kadhalika. Namba zilizo katika mabano zinawakilisha namba za mashairi. Pia kitabu hiki kina mashairi aina ya tathilitha (yaani yenye mishororo (mistari 3) mashairi hayo ni kama vile "Hali halisi" (3), "Puuzi" (5) Ua (3) "Kuunge" (16), na kadhalika.

Aidha yapo mashairi aina ya takhimisa yaani yenye mishororo (mistari mitano). Mfano "Siharakie Maisha" (7) na Israfu (11).

Mwandishi pia ameandika shairi la aina ya tasdisa lenye mistari 6. mfano ni shairi la 14 la "Punda."

Pia, yapo mashairi yenye mistari 11 ambayo yanajulikana kama mashairi ya usasa au mashairi ya vina, masivina.

Katika mistari inayounda beti, mwandishi ameyagawa katika vipande tofauti tofauti. Mfano wa vipande viwili ni "Mkulima:"

*Si leo toka zamani, mkulima mtu duni,*
*Ana tabu maishani,tena hapewi thamani*

Mifano mingine ni "Hali halisi," "Bahari, Puuzo," na kadhalika.

Pia, ipo mishororo (mistari) yenye vipande vitatu, mfano ni shairi la 1 "Kwa Nini:"

*Wanaume, nauliza, mwafanyani?*
*Pakashume, jigeuza, ni kwa nini*
*Mungurume, chezacheza, majiani*
*Kwa nini? (Ub.1).*

Shairi lingine lenye mishororo inayojengwa na vipande 3 ni "*Tunzo*" (19).

*Leo ninalo tamko, baada ya kuinama, kama tunzo,*
*Kwa hii misukosuko, kwenea dunia nzima, angamizo,*
*Nyoyo zina masumbuko, baraka zimetuhama, kwa puuzo.*

Mashairi mengine yenye mishororo yenye vipande vitatu ni pamoja na *"Haki"* (30) na kadhalika. Hata hivyo, mingi ya mishororo katika beti imejengwa kwa vipande viwili.

**MIZANI**

Mashairi yake yamejengwa kwa mizani tofauti tofauti. Baadhi ya mashairi yana mtindo usiozoeleka wa kuwa na mizani zaidi ya 16. mifano ya mashairi hayo ni *"Haki"* (30).

H a k i  w a t u t i s h a ,  t u s i k u a n d a m e ,  k w a  m a t e n d o  y e t u
1 2  3 4 5 6  7 8 9 10 11 12  13  14 15 16 17 18

W a t u k o r o f i s h a ,  t u s i a n d a m a n e ,  k i  l a  p e n y e  k i t u
1 2 3 4 5 6  7 8 10 11 12  13 14 15 16 17 18

M b o n a  w a t u n g w i s h a  m i l a  i t u c h o m e ,  k w e n y e  h u u  m w i t u
1 2 3 4 5 6  7 8 9 10 11 12  13 14 15 16 17 18

T u t o k w e  n a  u f u
1 2 3 4 5 6

Shairi jingine ni lile la *"Tunzo"* lenye mizani 20 kwa kila mshororo.

Le o ni na lo ta m ko, ba a da ya ku in a ma,
1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16
Ka ma tu nzo
17 18 19 20

Kwa nini misukosuko, kueneea dunia zima, angamizo nyoyo zima masumbuko, baraka zimetuhama, kwa puuzo.

Aidha, yapo mashairi yenye mishororo inayojengwa kwa mizani chache kuliko ilivyo kawaida. Mishororo ya namna hii ni ile inayofanya kazi ya kituo kwa mfano shairi la 26 la *"Ulimwengu."*

*Fikira zimekupaa, raha huna asilani,*
*Maungo yameshupaa, mifupa ihadharani,*
*Hebu nainge taa, ukweli utabani,*

U li mwe ngu!
1 2 3 4

Mfano mwingine ni ule wa shairi la "*Kwa nini?*" Kituo cha kila ubeti kimejengwa kwa mizani 3.

*Wanaume, nauliza, mwafanyani?*
*Paka shume, jijiuze, ni kwa nini?*
*Mungurume, chezacheza, majiani?*
*Kwa nini?*
1 2 3

**VINA**

Mashairi yake mengi yana vina vya kati na vya mwisho. Mfano, shairi la 8 "*Adui.*"

Haya shime tuitane, sote tushirikiane,
Wala tusitegeane, kwa pamoja tushikane,
Aliye mwoga anene, kabisa tusigombane,
Tutie jembe mpini, tuteremke shambani,

Mashairi yaliyojengwa kwa vipande vitatu hayo yana vina 2 vya kati na vya mwisho mfano shaini la "*Kwa Nini?*"

Utamwona, mwanaume, kashaini
Anong'ona, na selume, chochoroni
Ndiolana, ajipime, japatani
Kwa nini?

Mashairi yenye mtindo wa tenzi yamejengwa kwa vina vya mwishto tu mfano utenzi wa "Payuka."

Nasikia makelele
Ya ngoma ile yalele
Kuimba na kupayuka

Mfano mwingine ni shairi la "Israfu"

Mali ulojichumia
Ni yako nakubalia
lakini kiangalia
Vipi unaitumia
Mwenzangu nakuusia, isirafu haifai.

Mfano shairi la 29 "Pasua Uwape Ukweli."

*Ambaye tumekuridhi, asili yetu ni moja,*
*Sukani tumekukabidhi, toka zama za mababu,*
*Cheleza lete jahazi, uwapashe wapashike,*
*Pasi kuwa na woga, viduhushi wachochezi,*
*Uyakabili mawimbi, midomo yao wafyate,*
*Na hizo zake tufani, virago vyao wafunge.*

*Zipoze bila muhali, wawafate bwana zao,*
*Kwa kupasua ukweli, visiwa vishuwarike,*
*Kutugawa kwa mafungu, neema iengezeke,*
*Hilo kwetu ni muhali, tufurahie maisha,*
*Si dini wala si rangi, au la hata kabila.*

Aidha, waandishi wameonyesha upekee katika mashairi yao mambo kadha wa kadha. Mfano ni ule mtindo wa kuweka kutenganisha vipande katika mshororo mmoja. Mfano shairi la "*Adui.*"

*Njaa ikituvamia, sote tutaangamia,*
*Hakuna cha kungoja,lazima kuizuia,*
*Si kitu cha kuchezea,mbona itatuumbua,*
*Tutie jembe mpini, tuteremeke shambani.*

Mashairi mengine yenye mtindo huu ni kama vile "*Mkulima,*" "Tuyazingatie Hayo," *punda, Ua, Samaki Mtungoni.* n.k.

Aidha, mwandishi ameonyesha upekee kwa kuwa na kituo chenye mizani chache kuliko mishororo yote. Mfano ni shairi *Kwa nini,* kituo chake kina mizani tatu. "*Kwa Nini?*"

1 2 3

Mashairi mengine yenye mtindo huu ni kama lile la "Raha" lina kituo cha kipande kimoja cha mshororo. "Hii si Raha Karaha."

**VITUO**

Baadhi ya mashairi yana kituo bahari, kituo kisichobadilika kwa kila ubeti mfano shairi "*Adui,*" kituo ni "Tutie Jembe Mpini, tuteremke shambani."

Kituo cha shairi la *"Israfu"* ni "Mwenzangu nakuusia, Israfu haifai."

Mashairi mengine yenye kituo bahari ni Ua (13), "Usiwe Bendera" (20), "Nipate Wapi Mwingine" (21), Hina Inapapatika (35) na kadhalika.

Aidha, yapo mashairi yenye kituo kinachobadilikabadili (kitoshelezi). Mfano, shairi la *"Tunzo," "Sukari," "Nini wanangu,"* na kadhalika.

Pia, mwandishi ana aina nyingine ya kituo, ambacho ni nusu bahari. Kituo kinabadilika upande mmoja tu. Mfano, "*Charuka.*" "Kabla hujapotea, charuka chacharukaka". Kituo hiki kinabadilika sehemu ya kwanza kwa kila ubeti; mfano (Ub. 2) "Safari yaendelea, charuka, chacharukaka", (Ub.3) "Mashaka yatukulia, charuka chacharukaka; na kadhalika.

Baada ya kuangalia muundo wa kitabu cha *Malenga Wapya* sasa tuangalie kipengele cha mtindo

**MTINDO**

Mtindo wa mashairi yaliyo mengi katika *Malenga Wapya* yana mtindo wa kimapokeo.

Mashairi haya yanafuata kanuni za urari wa vina na mizani, mistari, n.k. Pia yapo mashairi machache yaliyo katika mtindo wa usasa. Mashairi haya ni yale yasiyo na ulinganifu wa vina na mizani, na yenye mistari zaidi ya sita. Mfano, ni shairi la "Haki" kituo chake kinajengwa kwa mizani 6.

Tu to kwe na u tu<br>1 2 3 4 5 6

Pia, mwandishi ameonyesha tofauti pale alipokuwa na kituo chenye mizani zinazokidhi haja ya ushairi katika utenzi. Mfano, shairi la *"Si harakie Maisha."*

Na ku o na wa du wa a<br>1 2 3 4 5 6 7 8

Ma i sha ku ya sha nga a<br>1 2 3 4 5 6 7 8

Hu su da zi na ku ja a<br>1 2 3 4 5 6 7 8

Ku hu su du li o ja a<br>1 2 3 4 5 6 7 8

Si ha ra ki e ma i sha, na we u na fu ngu la ko<br>1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16

Mashairi mengine yenye mtindo huu ni kama vile *"Israfu."* Washairi wameyapa namba mashairi yao, mfano 32 *"Payuka."*

## MATUMIZI YA LUGHA

Waandishi wametumia lugha fasaha kwa sehemu kubwa, na vilevile, kuna lugha ya msinyazo/mkato. Waandishi wamekatisha maneno ili kutia uzito wa jambo wanaloliongelea, kwa mfano, katika ubeti wa 7 shairi la "Israfu" mstari wa 3 kuna neno "Wache" badala ya "Waache". Pia neno "tajijutia" ubeti wa 7 shairi hilo hilo badala ya "Utajijutia".

Aidha, mwandishi ameipamba lugha yake kwa vionjo mbalimbali kama vile methali, misemo na tamathali za semi.

**Methali**
- Subira yavuta heri (shairi la 7, Ub. 8)
- Aisifue mvua kaloa mwilini mwake (shairi la 23, Ub. wa 12)
- Fahali wapiganapo nyasi ndizo huonewa (shairi la 37, Ub.7)

**Misemo**
- Siharakie maisha (shairi la 7)
- Kusumbukia kichaa (shairi la 23)
- Sokomoko baharini (shairi la 37)
- Kupanda mori (shairi la Maisha ni kama njia (Uk.40) Ub.1, mst. wa1)

**Tashbiha**
- Ubaguzi umezama kama nguo (shairi la 19, Ub.4)
- Maisha ni kama njia (shairi la 24)
- Mfanowe kama radi chini inapoanguka
- Nikabaki kama ngonda (shairi la Nipatieni Dawa (Uk.35) Ub. 6)
- Yameotewa na kombe mithili ya gome la mti (shairi la Bahari Ub. wa 2, mst. wa 3)
- Ruka vikwazo ja panzi (shairi la Siharakia Maisha (Uk.11) Ub. 2, mst. wa 3)

**Tashtiti**
- Nasikia mnatunga, mwatungani washairi? (shairi la 36 "Mwabaja Mwasema Nini?")

**Tashhisi**

Vitu visivyo na uhai vinapewa uwezo wa kutenda kama viumbe binadamu.
- "Samaki Mtungoni" – shairi la 12 samaki wamepwa uwezo wa kibinadamu. Mf. Ub. 6, mstari wa 1. "Samaki wasikitika, kudai walikotoka." (Uk. 46)

- Cheleza lete jahazi (shairi la Pasua uwape ukweli, Ub.1, mst. wa 3).
- Ndevu kuchomana shairi la *"Haki"* Ub. 4, mst. wa 3)
- Bahari ina aibu shairi la *"Bahari"* ub. wa 3, mst. wa 2)
- Majabali yenye pembe, yasimama madhubuti shairi la Bahari ub. wa 2, mst. wa 2)

**Sitiari**

Ulinganifu wa vitu bila kutumia viungansihi:
- "Ulimwengu ni shetani" katika shairi la *"Ulimwengu"* (Ub. 4, mst. wa 3)
- "Haki watutisha" shairi la *"Haki"* (Ub.1, mst. wa 1)

**Takriri**

Tendo la kurudiarudia neno au silabi kwa lengo la kusisitiza
- "Hai hati hai hati" shairi la *"Ulimwengu"* (Ub.6, mst. wa 3)
- Usiropoke ropoke shairi la *"Ulimi"* (Ub. 3, mst. wa 1)
- Charuka chacharukaka katika shairi la *"Charuka"*(Uk.53)

**Tanakali sauti**
- Kokoriko mitaani shairi la *"Mkulima"* (Ub. wa 2, mst. wa 1)
- Parakacha (shairi la *"Kwa nini"*?) Ub.4 mst. wa 22.

**Nahau**
- Nipate ufueni ikiwa na maana nipate nafuu (shairi la 22 *"Nipatieni Dawa"* Ub.9, mst. wa 3).
- Usiwe bendera maana yake usiwe mtu wa kufuata kila unachoambiwa au elekezwa (shairi la *"Usiwe bendera"* Ub. 1, mst. wa 4).

**Lugha ya Picha**
- Picha nyingi zimetumika ili kuipa mvuto kazi hii. Mfano, shairi la 12 *"Samaki Mtungoni"* kuna picha ya 'samaki', picha ya 'mvuvi' kukasirika; n.k. Shairi la *"Kitendawili"*, kuna picha ya 'jogoo', 'mbwa', n.k.

Katika shairi la *"Ua"*, kuna picha ya 'ua' linaloningi'nia mtini. Taswira zinazojengwa na picha hizo zitafafanuliwa kwenye kipngele cha taswira.

**Taswira**

Mwandishi ametumia picha zinazojenga taswira mbalimbali. Baadhi ya taswira hizo ni:

- Njiwa, yenye maana ya mpenzi (shairi la "*Nipate wapi Mwingine*")
- Samaki, yenye maana ya watu wa tabaka la chini (shairi la "*Samaki Mtungoni*")
- Mvuvi yenye maana ya watu wa tabaka tawala (shairi la "*Samaki Mtungoni*")
- Punda, yenye maana ya tabaka la chini linalonyonywa na kugandamizwa (shairi la "*Punda*")
- Ua, yenye maana ya msichana au mwana mke (shairi la "*Ua*").

**KUFAULU KWA WAANDISHI**

Kufaulu kwa waandishi kunatathminiwa kimaudhui na kifani. Waandishi wamefanikiwa kuonyesha dhamira mbalimbali ambazo zinajitokeza katika maisha yetu ya kila siku.

Aidha, wameonyesha mvutano baina ya tabaka la chini na la juu (uongozi mbaya).

Waandishi wamefanikiwa kifani kwa kutumia lugha ya kishairi nyepesi na yenye matumizi ya picha na taswira.

**KUTOFAULU KWA WAANDISHI**

Katika mashairi ya "*Mkulima*" na "*Adui*" waandishi wameonyesha ukasuku walio nao tangu zama za mababu, watu walikuwa wakilima lakini bado hali zao ni duni. Aidha, wamekuwa wakirudiarudia maneno yanayoimbwa majukwaani kuhusu viongozi badala ya kutuonyesha njia za kisayansi na kiteknolojia za kuondokana na matatizo ya kiuchumi, kifikra na kijamii.

Pia, wasanii wamekuwa na mtazamo potofu na dhaifu katika kutoa baadhi ya maadili, mfano Shairi la "*Hisani hulipwa.*"

**Kutofaulu kifani**

Mashairi haya yametumia lugha rahisi kiasi kwamba haimfikirishi sana msomaji.

### 12.3.8 ZOEZI LA PILI

*Jibu maswali yafuatayo kisha linganisha majibu yako na yale yaliyotolewa katika kijitabu hiki*

1. Somo shairi hili kisha jibu maswali yanayofuatia:

**"Ulimi"**

"Ulimi ninakuasa, nisemayo usikie,
Mwenzio sijenitosa, nafasi sijijutie,
Ninachokuomba hasa, unifanye nivutie,
Ewe ulimi sikia.

Usijenipa machungu, na watu huwarukia,
Sitengane na wenzangu, na wao kunichukia,
Hayo yapo juu yangu, usemapo yasonjia,
Ewe ulimi sikia.

Usiropokeropoke, kwa wenzio kwanza sema,
Usipachike pachike, maneno yasiyo maana,
Useme wanufaike, kwa kauli yako njema,
Ewe ulimi sikia."

(a) Shairi hili lina mizani ------------------------------------

(b) Katika ubeti wa kwanza kina cha kati ni ----------------
kina cha mwisho ni ----------------------------------------

(c) Tamathali zilizojitokeza katika shairi hili ni ------------

Shairi hili lina mistari mingapi kila ubeti? Shairi lenye mistari kama hiyo linaitwaje? -----------------------------------

2. Lugha iliyotumika katika Kitabu cha *Malenga Wapya* ni ya namna gani?
------------------------------------------------------------------
------------------------------------------------------------------

3. Katika kitabu cha *Malenga Wapya* lugha ya picha imetumika, toa mifano kwa kifupi.
------------------------------------------------------------------
------------------------------------------------------------------

## 12.3.9 MUHTASARI WA SEHEMU YA PILI

Fani ya kitabu cha *Malenga Wapya* imejumuisha muundo, mtindo na matumizi ya lugha na mandhari. Kimuundo mashairi ya Malenga Wapya mengi ni ya aina ya tarbia (mistari minne). Aidha yapo ya tathilitha (mistari mitatu), takhamisa (mistari mitano), tasbsa (mistari sita) na yale ya muundo wa masivina yaani yenye mizani saba na kuendelea.

Mashairi mengi yana mizani 16. Hata hivyo, yapo yenye mizani 18, na 20. Shairi lenye beti chache katika kitabu cha *Malenga Wapya* lina ubeti mmoja na shairi lenye beti nyingi lina beti 17.

Waandishi wametumia vina vya kati na vya mwisho katika mashairi yao mengi.

Vituo vilivyojitokeza katika kitabu cha *Malenga Wapya* ni kituo bahari, nusu bahari na kituo kinachobadilika kwa kila ubeti (kitoshelezi).

Waandishi wa *Malenga Wapya* wanatumia mtindo wa kimapokeo katika mashairi yao mengi. Hata hivyo, mashairi yenye mtindo wa usasa yametumika pia.

Matumizi ya lugha katika kitabu cha *Malenga Wapya* yamejumuisha mbinu mbalimbali kama vile, matumizi ya lugha ya picha, taswira, methali, tamathali za semi, nahau, misemo, n.k.

Mandhari ya kitabu hiki ni ya Unguja na kwingineko kokote katika ulimwengu wa tatu.

### 12.3.10 MASWALI YA KUTUMA KWA MKUFUNZI

*Jibu maswali yafuatayo kwenye kitabu cha mazoezi ulichopewa kisha kitume kwa Mkufunzi kwa masahihisho.*

1. Waandishi wa Malenga Wapya wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuelimisha jamii katika masuala ya uchumi, afya na ukombozi. Jadili ukweli wa kauli hii.

   **[Alama 20]**

2. Lugha ni nyenzo muhimu katika kazi yoyote ya kifasihi. Onesha matumizi ya lugha katika kitabu cha *Malenga Wapya.*

   **[Alama 20]**

3. Jadili dhamira ya ndoa na mapenzi kama ilivyojadiliwa na Waandishi wa Kitabu cha *Malenga Wapya.*

   **[Alama 20]**

4. Onesha mbinu za kifani zinazojenga mashairi ya Malenga Wapya.

   **[Alama 20]**

5. Miongoni mwa kazi za kisanii ni kuweka wazi maovu yaliyojificha na kuyakemea. Ni kwa vipi wasanii wa Malenga Wapya wametekeleza wajibu huo.

   **[Alama 20]**

### 12.3.11 MUHTASARI WA SOMO LOTE

Kwa ujumla, wasanii wa *Malenga Wapya* wamejadili kwa kina masuala mbalimbali yaihusuyo jamii. Wamejadili dhamira ya kuinua uchumi, uongozi mbaya, nafasi ya mwanamke, maadili mema ukombozi, mapenzi na ndoa, haki, matumizi bora ya mali (pesa), umuhimu wa kutatua matatizo na athari za sukari mwilini. Haya ni baadhi tu ya masuala yaliyopo katika jamii ya leo kwani ni mengi sana. Aidha, mashairi yaliyohakikiwa yana uwezo wa kujadili masuala zaidi ya moja kulingana na uhalisia wa lile lizungumzwalo katika mazingira halisi.

Pia, kwa upande wa ujumbe tumejifunza kuwa kuinua uchumi ni jambo muhimu sana ili kuondokana na utegemezi wa misaada toka nje. Pili, kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wetu hivyo hatuna budi kukiimarisha na kumthamini mkulima; kuwa ukombozi wa mwanamke ni suala muhimu sana ili aweze kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa jamii; kuwa ni muhimu kutatua matatizo mbalimbali yanayoikabili jamii ili kuweza kuishi kwa amani na utulivu; kuwa ni vizuri kuwa na maadili mema katika jamii ili kujenga jamii yenye haki na usawa; kuwa ili kujiletea maendeleo tuepukana na utumiaji ovyo wa mali tuipatayo. Mwisho, viongozi wanapaswa kuwa watendaji kwa vitendo na sio wapiga porojo za majukwaani.

Kwa upande wa fani, tumejifunza kuwa mwandishi ametumia lugha nyepesi na fasaha yenye utajiri wa tamathali za semi, misemo, nahau, lugha ya picha na tawira mbalimbali. Aidha, muundo wa mashairi katika *Malenga Wapya* ni ule wa tarbia. Pia, yapo mashairi ya muundo wa tathlitha (mistari 3), takhmisa (mistari 5), tasidisa (mistari 6) na yenye mistari zaidi ya sita lenye kueleweka kama shairi la kisasa au masivina. Shairi lenye beti chache lina ubeti mmoja na lile lenye beti nyingi lina beti kumi na saba (17). Mashairi yaliyo mengi yana mizani kumi na sita. Hata hivyo, yapo mashairi yenye mizani kumi na nane na ishirini. Mashairi mengi yana vina vya kati na vya mwisho.Vipo vituo bahari, nusu bahari na vituo vinavyobadilikabadilika kila ubeti (kitoshelezi).

Vilevile, waandishi wa *Malenga Wapya* wametumia mitindo yote miwili ya mashairi ya kimapokeo na yale ya kisasa.

Mandhari ya *Malenga Wapya* ni ya Unguja na kwingineko katika ulimwengu wa tatu (nchi zinazoendelea).

## 12.3.12 MAJIBU YA MAZOEZI

### Zoezi La Kwanza

1. Dhamira
   - kuinua uchumi
   - uongozi mbaya
   - nafasi ya mwanamke
   - maadili mema
   - haki
   - umuhimu wa kutumia mali vizuri
   - umuhimu wa kuondoa matatizo katika jamii
   - athari za sukari mwilini
   - mapenzi na ndoa

2. Mafundisho
   - Ni muhimu kuinua uchumi wa nchi ili kuondokana na utegemezi wa misaada toka nje.
   - Kilimo ni uti wa mgongo wa nchi yetu, hivyo lazima tukiimarishe na kumthamini mkulima.
   - Ukombozi wa mwanamke ni suala muhimu sana ili aweze kushiriki kikamilifu katika kujiletea maendeleo.
   - Ni muhimu kutatua matatizo yanayoikabili jamii ili kuweza kuishi kwa amani na utulivu.
   - Ni vizuri kuwa na maadili mema katika jamii ili kujenga jamii yenye haki na usawa.
   - Ili kujiletea maendeleo ya kudumu tuepukane na ufujaji wa mali.
   - Viongozi wawe watendaji kwa vitendo na sio wapiga porojo majukwaani.

3. Matatizo ya nchi: anguko la uchumi, maradhi na ujinga.

**Zoezi la Pili**

1. (a) Shairi la "Ulimi" lina mizani 16

   (b) Katika ubeti wa kwanza kina cha kati ni 'sa', na kina cha mwisho ni 'le'.

   (c) Tamathali zilizojitokeza katika shairi hili ni – takriri, silabi e, sa ubeti wa kwanza 'ngu' – 'a' ubeti wa pili 'ke', 'a' ubeti wa tatu.

2. Lugha iliyotumika katika Kitabu cha Malenga Wapya ni ya kawaida, inaeleweka kwani ni fasaha. Aidha, kuna matumizi ya msinyazo, msanii amekatiza baadhi ya maneno ili kutia uzito wa jambo analoliongelea. Mfano, ubeti wa 2 katika shairi la ULIMI "Sijenitosa" badala ya usije kunitosa.

3. Katika kitabu cha Malenga Wapya lugha ya picha imetumika mfano shairi "Nipate wapi mwingine" picha njiwa ina maana ya mpenzi. Picha ya "Ua" ina maana ya mwanamke (Mpenzi).

### 12.3.13 MAREJEO

Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni Zanzibar, 1991 Malenga Wapya,Kituo cha EWW Zanzibar.

Nyangwine, N. C. Ranyuma, S. Y, 2004. Tahakiki vitabu Teule vya Fasihi Kidato cha 34, Afroplus Industries Ltd, Dar es Salaam.

**TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA**
**ELIMU MASAFA NA ANA KWA ANA**


**Somo Limetwaliwa na:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| - | Consolata Mushi | - | BAKITA |
| - | Pachal J. Mulimanyi | - | Shule ya Sekondari Jangwani |
| - | Devota Theobald | - | Shule ya Sekondari Kisutu |
| - | Bruno Mganga | - | Shule ya Sekondari Azania |
| - | Mary Kimaty | - | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |

**Somo Limehaririwa na :-**

| | | | |
|---|---|---|---|
| - | Lucy Mlazi | - | (Mhariri Mkuu) Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |
| - | Saifu Kiango | - | Tanzania Publishing House |

**Waratibu:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| - | Athumani Mauya | - | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |
| - | Leonard Katoba | - | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |



© Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima 2006



**TOLEO LA PILI**

Namba ya Somo zima ISBN 9976 68 066 x

Namba ya Moduli hii: ISBN 9976 68 067 3

Limechapwa na Kiwanda cha Uchapaji
Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima